

Utangulizi wa chapisho la nne

Bhante S. Dhammika Imetafsiriwa na Elijah Ogeda"

Imetafsiriwa na Elijah Ogeda

Miaka kumi na nane zilizopita kundi la wanafunzi wa Ubuddha kutoka shule kikuu cha Singapore walikuja kwangu wakilalamika kwamba walipata ni vigumu sana kwao kujibu maswali kuhusu Ubuddha ambazo watu saa zingine waliwauliza. Niliwaambia wanipatie mifano ya baadhi ya maswali haya na walipofanya hivyo, nilishangazwa kwamba wanafunzi werevu hawa waliojifunza walijua machache sana kuhusu dini yao na kuwa na upuuzi wa kuieleza kwa wengine. Nilitia maanani haya maswali mengi, nikaongeza zingine ambazo mara kwa mara niliulizwa na hivyo ndivyo Swali nzuri Jibu nzuri likawa. Kile ambacho kilikuwa kitumiwe na wana Singapore, kwa mshangao wangu na kuridhishwa kwangu, kimekuwa kisomi cha kimataifa. Chapisho 150,000 ya lugha ya Kingereza zimechapishwa na kutolewa mara kadhaa Marekani, Malaysia, India, Thailand, Sri Lanka, na Taiwan. Pia imetafsiriwa kwa lugha 14, hivi karibuni kwa Bahasa, Indonesia, na Kihispania. Katika chapisho hili la nne lililoimarishwa na kuwa na maelezo zaidi nimeongeza maswali mengi na pia nimepatiana, natumaini majibu mazuri kwa hayo maswali. Pia nimeongeza sura mpya ambayo ina misemo kuhusu Buddha. Ningependa kumshukuru Lee Teng Yong kwa kusaidia kuandaa hiki chapisho kipyua. Hiki kijitabu kidogo kiendeleo kuwa changamoto katika Dhamma ya Buddha.

S. Dhammika

Singapore, 2006

1.UBUDDHA NI NINI?

SWALI: Ubuddha ni nini?

JIBU: Jina Ubuddha linatoka kwa neno *budhi* ambayo lina maanisha ‘kuamka’ na kwa hivyo Ubuddha inaweza semwa ni filsofia ya kuamka. Hii filsofia lina asili yake kutokana na aliyoyapitia Siddhattha Gotama, ambaye ni Buddha, aliye amshwa akiwa umri wa miaka 35. Ubuddha kwa sasa lina miaka 2500 na ina wafuasi milioni 380 ulimwenguni kote. Mpaka miaka mia moja uliyopita Ubuddha ulikuwa filsofia kutoka Asia lakini waamini wake wanaongezeka Uropa, Australia na Marekani.

SWALI: Kwa hivyo Ubuddha ni filsofia tu?

JIBU: Neno filsofia linatoka kwa maneno mawili, *filo* ambayo ina maanisha ‘upendo’, na *sofia* inayo maanisha ‘hekima’. Sasa filsofia ni upendo wa hekima ama upendo na hekima, maana yote kufafanua Ubuddha vizuri. Ubuddha inatufundisha ya kwamba tunafaa tujaribu kuyaendeleza fikra zetu ili tuweze kuelewa vizuri. Pia inatufundisha kuendeleza upendo na ukarimu ili tuweze kuwa kama marafiki wa kweli kwa viumbe vyote. Sasa Ubuddha ni filsofia na sio filsofia tu. Ni filsofia ya kiwango cha juu.

SWALI: Buddha alikuwa nani?

JIBU: Mwaka 563 BC mtoto alizaliwa kwa familia ya ufalme kaskazini mwa India. Walimlea kwa mali na raha lakini aligundua ya kwamba anasa za dunia na usalama hazikumahidi furaha. Kwa undani alisukumwa na mateso aliyoyaona kwa mazingira yake na kuamua kutafuta ufunguo wa furaha. Alipokua umri wa miaka 29 alimwacha mkewe na mtoto akaenda kukaa na walimu wa dini wa nyakati hizo ili kujifunza kutoka kwao. Walimfunza mengi lakini hakuna aliyejua kwa uhakika chanzo cha mateso ya binadamu na jinsi ya kuzitatua. Baada ya miaka sita ya kujifunza, kujimudu na kuwaza, alipitia mapito ambayo dhuluma zote yaliisha na hatimaye alielewa. Kuanzia hiyo siku aliitwa Buddha, aliye amka. Aliishi kwa miaka 45 mengine aliporudi kaskazini mwa India akiyafunza yale ambayo aliyoyagundua. Huruma na utulivu wake ilikua ya ushujaa, alikuwa na maelfu ya waamini. Katika miaka yake ya themanini, akiwa mzee na mgonjwa, na kuheshimiwa, aliaga dunia.

SWALI: Je, ilikuwa utovu wa nidhamu Buddha alipomwacha mke wake na mtoto?

JIBU: Haingekuwa kitu rahisi sana kwa Buddha kumwacha familia yake. Huenda angekuwa na wasiwasi na kutofanya hivyo kwa muda mrefu kabla ya kuamua kuondoka. Lakini alikua na uamuzi, ajitolee kwa familia yake ama kwa ulimwengu. Mwishowe, ukarimu wake ulimfanya kujitokelezea kwa ulimwengu nzima na ulimwengu nzima bado inanufaika kwa kujitokelezea kwake. Hii haikuwa utovu wa nidhamu. Ilikuwa pengine kujitokelezea muhimu lililoweza kutendwa.

SWALI: Kama Buddha amekufa anaweza kutusaidiaje?

JIBU: Faraday aliye anzililisha umeme amekufa, lakini uzinduzi wake bado inatusaidia. Luis Pasteur aliyezindua matibabu ya magonjwa mengi pia amekufa, lakini uzinduzi wake bado inatusaidia. Leonardo da Vinci aliyekuwa msani wa sanaa amekufa lakini sanaa zake zinaweza inua moyo na kuleta furaha. Mashujaa wengi wanaweza kuwa wamekufa kwa mia za miaka lakini tunaposoma walioyafanya na manufaa walioyapata, bado tunaweza iga mifano yao na kufanya kama walivyoyafanya. Ndio, Buddha amekwisha kufa, lakini miaka 2500 baadaye mafunzo yake bado inasaidia watu. Ni Buddha tu anayeweza kuwa na nguvu kama hiyo makarne baada ya kifo chake.

SWALI: Buddha alikua ni mungu?

JIBU: Hapana, hakuwa. Hakusema ya kwamba alikua mungu, mwana wa mungu ama mtumishi kutoka kwa mungu. Alikua binadamu aliyejiamsha na kufunza kwamba tuki iga mfano wake sisi pia tunaweza kujiamsha.

SWALI: Kama Buddha hakuwa mungu mbona watu wanamabudu?

JIBU: Kuna njia tofauti za kuabudu. Watu wanapomabudu mungu, wanamshangilia, wanatoa sadaka na kuomba wapate kusikizwa. Wana amini mungu atasikiliza shangilio zao, apokee sadaka zao na kujibu maombi zao. Mabuddha hawa abudu katika njia hii. Njia nyingine ya kuabudu ni tunapo onyesha ishara ya heshima kwa mtu ama kitu kinacho pendeza. Mwalimu aingiapo darasani tunasimama, tunapokutana na mtu muhimu tunasalamiana kwa mikono, na nyimbo ya taifa linapochezwa tunapiga saluti. Haya yote ni njia za kuabudu, kutamani na heshima. Hii ndio aina ya kuabudu ambayo Mabuddha wanajifunza. Sanamu ya Buddha na mikono zake zikiwa kwenye paja zake na furaha nyusoni inatukumbusha kuendeleza amani na upendo ndani yetu. Manukato ya ubani inatukumbusha kuhusu manufaa ya talanta, taa inatukumbusha kuhusu mwangaza wa kujifunza na maua, ambayo yanakauka na kufa inatukumbusha kuhusu kotokuwa. Tunapoinama tunaonyesha ishara ya shukrani kwa Buddha kwa mafunzo ambazo ametupatia. Hii ndio maana ya kuabudu kwa Mabuddha.

SWALI: Lakini nimesikia watu wakisema Mabuddha wana abudu sanamu?

JIBU: Misemo kama haya yana angaza kutoelewa kwa wale wanaozisema. Kamusi linafafanua sanamu kama kiumbe kisicho hai linalo abudiwa kama mungu. Vile mmeona, Mabudha hawaamini kwamba Buddha alikuwa mungu, sasa wanawezaje amini ya kwamba mbao ama chuma lililochongwa ni mungu? Madhehebu zote wanatumia ishara kuonyesha imani zao. Kwa Taoism, mchoro wa ying-yang inaonyesha amani kwa wasiosikizana. Kwa Sikhism, panga lina ishara ya vita za kiroho. Kwa Ukristo samaki inatumiwa kuonyesha uwepo wa kristo na msalaba kuonyesha kujitolea kwake. Kwa Ubuddha, sanamu ya Buddha inatukumbusha utofauti kwa binadamu kupitia mafunzo zake, ukweli kwamba Ubuddha ina angazia ubinadamu na sio kwa mungu, na kwamba inafaa tuangalie kwa undani, sio kwa uwezo na kuelewa. Kwa hivyo, kusema ya kwamba Mabuddha wana abudu sanamu ni ujinga kama kusema wakristo wana abudu samaki ama michoro.

SWALI: Mbona watu hufanya vitu vyote vya ajabu katika hekalu za Ubuddha?

JIBU: Vitu mingi vinaonekana vya ajabu tusipoyaelewa. Badala ya kuamua ya kwamba haya vitu ni vya ajabu, inafaa tujaribu kuyaelewa maana zao. Hata hivyo, ni kweli ya kwamba vitu vingine ambazo Mabuddha wanafanya, lilitoka kwa kushuku na kutoelewa kwa mafunzo ya Buddha. Na kutoelewa kama haya hayapatikani kwa Ubuddha pekee yake lakini yameingia katika dini zote mara kwa mara. Budha alifunza kwa ukweli na kwa undani na kama watu wengine wanakosa kumwelewa, makosa sio yake. Kuna msemo kwenye mandiko la Ubudha:

'Kama mtu ana ugua kwa ugonjwa na hamtafuti muuguzi hata kama muuguzi yupo, sio makosa ya muuguzi. Kwa njia sawa, kama mtu ana ugonjwa wa kufanya mambo mabaya na kutotafuta usaidizi wa Buddha, hiyo siyo makosa ya Buddha.

Jn. 28-9

Ubuddha ama dini yeyote haifai kukuhukumiwa na wale wasioyajifunza vizuri. Kama unataka kujua mafunzo ya kweli ya Ubuddha, soma maneno ya Buddha ama ongea na wale wanayoielewa vizuri.

SWALI: Kunayo siku kuu kwa Mabuddha kama Krismasi?

JIBU: Kulingana na mila, Siddhattha alizaliwa, akawa Buddha na akafa Siku kuu ya mwezi mzima ya Vesakha, mwezi wa pili ya kalenda ya India ambayo ilikuwa Aprili-Mei

ya kalenda ya ulaya. Siku hiyo Mabuddha wote nchini wanasherekea matukio haya kwa kuenda kwa hekalu, kuwa na sherehe mbali mbali ama kuchukua siku nzima wakitafakari.

SWALI: Kama Ubuddha ni nzuri sana, mbona nchi za Ubuddha zina umaskini?

JIBU: Kama kwa umaskini unasema umaskini ki uchumi, basi ni kweli ya kwamba nchi zingine za Ubuddha zina umaskini. Lakini kama kwa umaskini una maanisha maisha yasiyo mazuri, basi nchi zingine za Ubuddha wanao utajiri. Marekani kwa mfano, ni nchi lililoimarika kiuchumi na pia ni nchi yenye nguvu lakini hali yake ya usalama imedorora sana ulimwenguni kote. Mamilioni ya watu wazee wametengwa na watoto wao na hufa kwa kutengwa kwa boma zao. Vita vya kinyumbani, dhuluma kwa watoto na utumizi wa mihadarati ni shida kubwa, na moja kati ya ndoa tatu huharibika. Utajiri kwa uwepo wa fedha lakini umaskini kwa kuhifadhi maisha bora. Sasa ukiangalia nchi za Ubudha za kimila, unapata hali tofauti. Wazazi hupewa heshima na watoto wao, hali ya usalama haijadorora sana, na ndoa pia havivunjiki na kujiua ni nadra. Mila kama utulivu, huruma, kukaribisha usiowajua, heshima kwa wote bado zipo. Nyuma ki uchumi lakini mbele kwa kuhifadhi hali nzuri ya maisha kuliko nchi kama Marekani. Hata hivyo, tukihukumu nchi za Ubudha kwa njia ya uchumi pekee yake, moja wapo ya nchi tajiri na tena lililoimarika kiuchumi ni Japan, mahali ambapo asilimia wengi ya wananchi wanajiita Mabuddha.

SWALI: Mbona hatuikii kazi za Uhisani zikitendwa na Mabuddha?

JIBU: Pengine ni kwa sababu Mabuddha hawaoni haja ya kujivunia kuhusu wema waliozitenda. Miaka mingi yaliyopita, kiongozi wa Mabuddha kutoka Japan Nikkho Nirwano alipokea tuzo la Templeton kwa kazi yake ya kukuza maelewano za kidini. Vilevile mtawa wa Ubudha kutoka Thai hivi karibuni alituzwa kwa kazi yake njema kati ya wanaotumia mihadarati. Mwaka wa 1987 mtawa mwingine kutoka Thai, Ven. Kantayapiwat alituzwa tuzo la amani ya watoto wa Norwegian kwa miaka zake mingi ya kuwasaidia watoto wasio na makao katika sehemu za mashambani. Na kuhusu kazi kubwa ya kijamii linalofanywa kati ya masikini na amri ya ubudha kutoka magharibi? Wamejenga mashule, vituo vya kujali watoto, zahanati na viwanda vya kujimudu kibinafsi maridhawa. Mabuddha huona usaidizi uliopewa kwa wengine kama maonyesho ya zoezi la dini kama tu vile dini zingine hufanya, lakini wana amini linafaa lifanywe kisiri na bila majivunio.

SWALI: Mbona kunazo aina tofauti za Ubuddha?

JIBU: Kuna aina mingi ya sukari - sukari kahawia, sukari nyeupe, sukari jiwe, sukari tamu lakini zote ni sukari na zote zina ladha tamu. Zinaondolewa kwa njia tofauti ili kuweza kutumiwa kwa njia tofauti. Ubuddha ni sawa: Kunayo Ubuddha Theravada, Ubuddha Zen, Ubuddha Eneo Safi (Pure Land), Ubuddha Yogacara, na Ubuddha Vajrayana. Lakini zote ni mafunzo ya Buddha na zote zina ladha sawa- ladha ya uhuru. Ubuddha ulikuja kwa njia tofauti ili kuwe na husika kwa utamaduni tofauti linakotoka. Imetasfiriwa kwa makarne ili iweze kuwa na husika kwa kizazi ujao. Kwa nje, aina tofauti za Ubuddha zinaweza onekana tofauti lakini kiini chao zote ni Vyeo Nne za Ukweli na Cheo cha Njia Nane Mara ya Ukweli. Dini zote kubwa, ikiwemo Ubuddha, zimegawanywa kwa mashule na madhehebu. Pengine tofauti kati ya Ubuddha na madini zingine ni kwamba shule tofauti zimehimili na kuwa kirafiki kuelekeza kwa nyingine.

SWALI: Kwa kweli unafikiria kwa kiwango cha juu kuhusu Ubuddha. Natarajia unaamini hiyo ndiye dini ya kweli na kwamba zingine zote ni za uongo?

JIBU: Hakuna mfwasi wa Buddha anaye elewa mafunzo ya Buddha anaye fikiria ya kwamba dini zingine ni za uongo. Hakuna aliye jitahidi kamili kutahini dini zingine kwa fikra lililofunguliwa anayeweza kufikiria hivyo. Kitu cha kwanza unachogundua unapochunguza dini tofauti ni yale ambayo zinazo kwa umoja. Dini zote zinakubali ya kwamba hali ya mwanadamu kwa wakati huu hauridhishi. Zote zinakubali ya kwamba ubadilifu wa mtazamo na mwenendo unahitajika ili hali ya mwanadamu iweze kuimarika. Zote zinafundisha maadili inayohusisha upendo, ukarimu, utulivu, na jukumu la kijamii na zote zinakubaliana uwepo wa baaadhi ya aina kabisa. Wanatumia lugha tofauti, majina tofauti, na ishara mbali mali ili kueleza mambo haya. Watu wanaposhikilia kwa fikra nyembamba kwa njia ambayo wanatafakari vitu kwa kutovumilia, fahari na ukweli wa ubinafsi huimarika.

Fikiria mwingereza, mfaransa, mchina na mwana Indonesia wote wakiangalia kikombe. Mwingereza anasema, “hiki ni cup.” Mfaransa anajibu, “hapana, sivyo. Ni tasse.” Halafu mchina anatoa maoni, “nyote mmekosea. Hii ni pei.” Hatimaye mwana Indonesian anasema, “wapumbavu wagani hawa. “Hii ni cawan.” Halafu mwingereza akaondoa kamusi na kuonyesha wengine akisema, “naweza kudokeza hii ni cup. Kamusi yangu inasema hivyo.” “Basi kamusi yako si sawa”, akasema mfaransa, “kwa sababu kamusi yangu inasema ni tasse”. Halafu mchina akatoa umashkara, “Kamusi yangu inasema ni pei na kamusi yangu ni miaka maelfu kuliko yako sasa inaweza kuwa sawa. Zaidi ya hayo, watu wengi wanaongea Kichina kuliko lugha yeyote, sasa inaweza kuwa pei.” Wakati wanapojadiliana kati yao, mtu mwingine akaja, akanywa kutoka kwa kikombe hicho halafu akawaambia wengine, “kama unaliita cup, tasse, pei ama cawan, kazi ya kikombe ni kubeba maji ili yaweze kuyanywa. Kunyweni na mwache kujadiliana, burudisheni kiu chenu.” Hii ndio mwenendo wa Ubuddha kwa dini zingine.

SWALI: Watu wengine husema, dini zote kwa kweli ni sawa. Utakubaliana nao?

JIBU: Dini ni matukio matata mbali mbali yasiyoweza kurejelewa na msemu kama huo. Mbuddha anaweza sema msemu huu ina vipengele vya uwongo na ukweli. Ubuddha hufundisha kuwa Mungu hayupo, kwa mfano, na Ukristo inafundisha yupo. Nafikiria ya kwamba hii ni utofauti muhimu. Hata hivyo, Kifungu kimoja kizuri kwenye Biblia inasema:

‘Kama naongea lugha ya watu na malaika lakini sina upendo, Mimi ni kama kengele inayopiga tu kelele. Kama ninao zawadi ya kutaabiri na kuelewa siri na elimu zote, na nikiwa na imani iliyo ya nguvu inayoweza kusukuma milima, na sina upendo, mimi ni kitu kibure. Nikiwapa fukara mali yangu yote na kusalimisha mwili wangu kwenye moto na sina upendo, sifaidiki kitu. Upendo ni utulivu, upendo ni ukarimu. Upendo hauna wivu, upendo hauna majivunio, hauna kiburi. Upendo hauna ufidhuli, hautafuti ubinafsi, hasira haumpati virahisi, haichapishi orodha ya mabaya yaliyotendwa. Upendo haufurahishwi na dhambi lakini hufurahishwa na ukweli. Hutetea, hutumaini, husubiri.’

1 kor. 13-7

Hii hasa ndicho Ubuddha hufunza – kwamba ubora wa mioyo zetu ni muhimu kuliko nguvu zetu za kawaida tulizonazo, uwezo wetu wa kutaabiri wakati ujao, ushupavu wa imani zetu, na ishara za fujo tutendazo. Sasa inapokuja kwa dhana na nadharia za theolojia, Ubuddha na Ukristo kwa kweli hutofautiana. Lakini inapokuja kwa ubora wa moyo, maadili na mwenendo, hufanana sana.

SWALI: Ubuddha ni kisayansi?

JIBU: Kabla ya kujibu swali hilo, ingekuwa bora kufafanua neno ‘sayansi.’ ‘Sayansi ni, kulingana na kamusi, elimu ambayo inaweza tendwa kwa mfumo, linalotegemea kwa kuona na kujaribu tendo na kuainisha sheria za kiasili, tawi la elimu kama hiyo, chochote kinachoweza fanyiwa utafiti kamili.’ Kunazo vipengele vya Ubuddha yasiyoweza patana na ufafanuo huu lakini kati ya mafunzo ya Ubuddha, vyeo Manne za ukweli, inawezekana. Mateso, Cheo cha Kwanza cha Ukweli, ni mapito yanayoweza kufafanuliwa, pitiwa na kupimwa. Cheo cha Pili cha Ukweli linasema mateso lina chanzo za kiasili, pupa, ambayo vilevile laweza fafanuliwa, pitiwa na kupimwa. Hakuna jaribio lililotendwa kueleza mateso kwa njia ya kutafazikia dhana na hadithi. Kulingana na Cheo cha Tatu cha Ukweli, mapito yamekwisha, sio kwa kumtegemea kiumbe kikuu, kwa imani na maombi, lakini kwa kuondoa chanzo chake. Hii inakubalika. Cheo cha nne cha ukweli, njia ya kukomesha mateso, mara moja, haina chochote kuhusu kutafizikia

lakini hutegemea mwenendo kwa njia maalum. Na mara moja tena, mwenendo ni kipimo wazi. Ubuddha hauoni kwa dhana ya kiumbe kikuu, kama sayansi, inaeleza asili na kazi za ulimwengu kwa istilahi ya sheria za kiasili. Haya yote yana onyesha hadharani kwa roho ya kisayansi. Mara moja tena, ushauri wa mara kwa mara wa Buddha ni tusiamini vitu kwa njia iliyopofuka, bali tuulize, tuchunguze, na kuuliza na kutegemea kwa mapito yetu, lina pete la kisayansi ndani. Katika *Kalama Sutta* yake maarufu Buddha anasema;

‘Usiende kwa ufunuo ama utamaduni, usiende kwa uvumi ama maandiko takatifu, usiende kwa tetesi ama mantiki tu, usiende kwa upendeleo kuelekeza dhana ama kwa uwezo wa mtu mwingine na haukubaliani na wazo hilo “ Huyu ni mwalimu wetu.” Lakini kama wewe mwenyewe unajua ya kwamba kitu ni kizuri, na kwamba ni mtajeni, na linasifiwa na wenye hekima na likitendwa na kuchunguzwa inatuelekeza kwa furaha, basi fuata kitu hicho.’

A.I, 188

Sasa tunaweza kusema ingawa Ubuddha si Kisayansi kamili, kwa kweli lina dhana ya kisayansi kwa hali ya juu kuliko dini yeyote. Ni muhimu ya kwamba Albert Einstein, aliyekuwa mwansayansi maarufu wa karne ya ishirini aliongea kuhusu Ubuddha:

Dini ya wakati wa ujao utakuwa dini sawa. Itaweza kuvusha Mungu wa kibinafsi na kuepokana na mafunzo za theolojia. Kufunika asili na kiroho zote, msingi wake utakuwa wa kidini na kutoka kwa mapito ya vitu vyote, za kiasili na kiroho na ya maana kiunganishi. Ubuddha unajibu fafanuo hili. Kama kunayo dini itakayo ambatana na mahitaji ya kisasa ya kisayansi, basi itakuwa ni Ubuddha.’

SWALI: Saa zingine nimesikia kuna funzo la Buddha liitwayo Njia Kati. Istilahi hii ina maanisha nini?

JIBU: Buddha alipeana Njia zake Nane Imara kwa jina lingine , *majjhima patipada*, inayo maanisha ‘Njia Kati.’ Hii ni jina muhimu kwa sababu inatuelimisha ya kwamba kufuata njia haitoshi, lakini inafaa tuifwate kwa njia maalum. Watu wanaweza kuwa watiifu kuhusu sheria za kidini na vitendo mpaka wakawa mashabiki wa kweli. Kwa Ubuddha sheria lazima zifwatwe, na vitendo vitendazwo vinatendwa kwa njia ya usawa na sababu kinachozuia ukithiri wa ziada. Nyakati ya Roma ya kale ilikuwa ikisema ‘wastani kwa vitu vyote’ na Mabuddha watakubaliana na hiyo kabisa.

SWALI: Nilisoma ya kwamba Ubuddha ni kama aina ya Uhindi. Hii ni kweli?

JIBU: La sivyo. Ubuddha na Uhindi zinashiriki maadili mengi, wanatumia istilahi fulani za kawaida kama *Kamma*, *Samadhi* na *Nirvana* na zote zina asili kutoka India. Hii imewaongoza watu wengine kufikiria ya kwamba ziko sawa au zinafanana. Lakini tukiangazia juu juu usawa haya tunaona ya kwamba dini zote mbili zina utofauti. Kwa mfano, Wahindi wana amini kwa Mungu mkuu na Mabuddha hapana. Moja kati ya mafundisho za filofia ya kijamii ya kihindi ni fikra ya caste, ambayo Ubuddha wanatupulia mbali. Ibada ya usafishaji ni shughuli muhimu kwa mhindi lakini haina nafasi katika Ubuddha. Katika maandiko ya Ubuddha Buddha anaonyeshwa akikosoa mafunzo ya Brahmins na Makasisi wa uhindi. Hatimaye walikihakiki mafunzo zake zingine. Hii haingefanyika ikiwa Ubuddha na Uhindi zingefanana.

SWALI: Lakini Buddha alinakili wazo la kamma kutoka Uhindi, sivyo?

JIBU: Uhindi haina mafundisho ya *kamma* na pia uwepo wa maisha baada ya kifo. Hata hivyo, mafunzo yao kuhusu mafunzo hizi ni tofauti na mafunzo ya Ubuddha. Kwa mfano, Uhindi inasema wana ujasiri kwa *kamma* yao na Ubuddha inasema *kamma* yao ina masharti. Kulingana na uhindi, nafsi milele ama atman inapitia maisha moja kuelekea kwa nyingine. Ubuddha hata hivyo inakataa uwepo wa nafsi kama hiyo wakisema afadhali ni mabadiliko ya mikondo ya kiakili lizaliwayo. Haya ni baadhi ya tofauti zilizoko kati ya dini hizi mbili kuhusu *kamma* na kuzaliwa tena. Hata hivyo, hata kama mafunzo ya Ubuddha na Uhindi zinafanana hii hainge maanisha ya kwamba Buddha alinakili kwa kutowaza wazo ya wengine. Saa zingine inatendeka kwamba watu wawili, wanaotoka mbali na mwingine, hufanya ugunduzi sawa. Mfano mzuri ni ugunduzi wa mageuko. Mwaka wa 1858, kabla ya kuchapisha kitabu chake maarufu ‘The Origin of the Species’, Charles Darwin aligundua kwamba mme mwingine, Alfred Rusell Wallace, alishakuwa na wazo la mageuzi kama alivyowaza. Darwin na Wallace hawakunakiliana mawazo. Badala ya hiyo, kwa kuchunguza matukio sawa, walifikia hitimisho sawa kuhusu. Sasa hata kama wazo ya Uhindi na Ubuddha kuhusu *karma* na uwepo wa maisha baada ya kifo zingefanana, ambayo siyo, hii haina dhibitisho kwamba kulikuwa na tukio la kunakili. Ukweli ni kwamba kupitia ufahamu waliendeleza kutafakari, Wahenga wa kihindi walipata mawazo mabaya kuhusu *kamma* na uwepo wa maisha baada ya kifo ambayo Buddha baadaye alifafanua kikamilifu na kwa uangalifu.

2. MSINGI WA DHANA ZA UBUDDHA

SWALI: Mafunzo makuu za Buddha ni gani?

JIBU: Mafunzo zote mengi za Buddha huangazia Vyeo Manne Makuu vya Ukweli vile gurudumu huwa kwenye kitovu. Zinaitwa ‘Manne’ kwa sababu yako manne. Zinaitwa ‘Vyeo’ kwa sababu zinamsababisha mtu kuzielewa. Na zinaitwa ‘ukweli’ kwa sababu, zinalingana na uyaakinifu, ni za ukweli.

SWALI: Cheo Kikuu cha Kwanza cha Ukweli ni gani?

JIBU: Cheo Kikuu cha Kwanza cha Ukweli ni kwamba maisha ni mateso. Kuishi ni kuteseka. Ni vigumu kuishi bila kupitia aina yeyote ya dhiki. Lazima tuvumilie mateso ya kifizikia kama ugonjwa, jeraha, uchovu, uzee na hatimaye kifo. Lazima pia tuvumilie mateso ya kisaikolojia kama upweke, kuchanganyikiwa, masikitiko, hasira, huzuni, na kadhalika.

SWALI: Si huo ni tamaa kiasi?

JIBU: Kamusi hufafanua tamaa kama ‘tabia ya kufikiria ya kwamba kitakachotendeka kitakuwa kibaya,’ ama imani kwamba ubaya unao nguvu kuliko uzuri.’ Ubuddha haufundishi mawazo kama haya. Aidha haikatai uwepo wa furaha. Kwa urahisi inasema kuishi ni kupitia mateso ya kifizikia na ya kisaikolojia ambayo ni msemu iliyo ya ukweli na usioweza kukataliwa. Ubuddha sio tamaa, inatufundisha kupambana na uyaakinifu wa kuwepo kwetu. Ubuddha huanza na pitio, ukweli usiopingwa, kitu ambacho wote hujua, ambacho wote wamepitia na kujaribu kuepuka. Hivyo, Ubuddha huanza kwa kuenda kiwimawima kuelekea kwa kiini ya wasiwasi ya kila mwanadamu – mateso na kuiepuka.

SWALI: Cheo kikuu cha pili cha ukweli ni gani?

JIBU: Cheo Kikuu cha Pili cha ukweli ni kwamba tamaa huleta mateso. Tunapoangazia mateso ya kisaikolojia, ni rahisi kuona vile inasababishwa na tamaa. Tunapotaka kitu na hatuwezi kuipata, tunasikia masikitiko ama kuchanganyikiwa. Kama tunatarajia kitu kwa mtu na hawafanyi kulingana na matarajio yetu, tunahuzunishwa na kukasirishwa. Tunapotaka kupendwa na wengine na hawatupendi, tunasikia vibaya. Hata tunapotaka kitu na hatukipati, hatuelekezwi kwa furaha kwa sababu sio muda mrefu kabla ya kuchoshwa na kitu hicho, kupoteza maslahi na kuanza kutamani kitu kingine. Ikiwekwa virahisi Cheo Kikuu cha Pili cha Ukweli linasema ya kwamba kile tutakacho haituahidi furaha. Badala ya kupambana kila wakati kupata utakacho, jaribu kurekebisha matakwa zako. Tamaa hutunyima kuridhishwa na furaha.

SWALI: Lakini tamaa na pupa hutuelekezaje kwa mateso ya kimwili?

JIBU: Maisha ya tamaa na pupa kwa hiki na kile, na sanasana tamaa ikiendelea kuwepo hujenga nguvu linalomfanya mtu kuzaliwa tena. Tunapozaliwa tena, tunakuwa na mwili na tulivyosema hapo awali, mwili huweza husishwa kwa jeraha na ugonjwa; inaweza kuchoshwa na kazi; huzeeka na hatimaye hufa. Hivyo, tamaa huelekeza kwa mateso ya kmwili kwa sababu inatusababisha kuzaliwa tena.

SWALI: Hivyo ni vizuri sana. Lakini tukiwacha kutamani hatuwezi kupata ama kutimiza kitu chochote?

JIBU: Ukweli. Lakini kile ambacho Buddha anasema ni kwamba wakati hamu zetu, tamaa zetu, kutoridhishwa kwetu ya kila mara, na matamano ya ziada hutusababisha kuteseka, basi inafaa tukome kutenda hivyo. Alitambia kuweka tofauti kati ya vitu tunavyohitaji na yale tunayoyataka, na kupambana kwa mahitaji na kerekebisha matarajio zetu. Alitufundisha kwamba mahitaji zetu zinaweza kutekelezwa lakini matarajio zetu ni shimo lisicho na ukingo. Kuna mahitaji ambazo ni muhimu, msingi ambazo zinaweza kupokelewa, na tunafaa kusughulika tuweze kuyatekeleza haya. Matamano ya ziada yanafaa kupunguzwa hatua kwa hatua. Hata hivyo, kusudi la maisha ni nini? Kupata, ama kuridhishwa na furaha?

SWALI: Umeongea kuhusu kuzaliwa tena, lakini kunazo ushahidi tosha ya kuwa kitu kama hicho hufanyika?

JIBU: Kunazo ushahidi tosha ya kuwa kitu kama hicho hufanyika lakini tutaiangazia kwa undani hapo mbeleni.

SWALI: Cheo Kikuu cha Tatu cha Ukweli ni gani?

JIBU: Cheo Kikuu cha Tatu cha ukweli ni kwamba mateso yanaweza shindwa na furaha kufikiwa. Hii pengine ni muhimu kwa hayo vyeo zote nne makuu za ukweli kwa sababu ndani yake Buddha anatuthibitishia ya kwamba furaha ya ukweli na kuridhika yanawezekana. Tunapoepushana kuishi kwa tamaa isiyo ya kufaa na kujifunza kuishi kila siku kwa wakati, kufurahia bila kutulia tamaa ambazo maisha inatuahidi, kupitia kwa utulivu shida ambazo maisha inatuhusisha nayo bila kuogofya, chuki na hasira, basi tunakuwa na furaha na uhuru. Hivyo na ni hivyo tu, ndivyo tunavyoweza kuishi kikamilifu. Kwa sababu hatufadhaishwi tena kwa kuyatimiza matakwa zetu za pupa, tunapata tunao wakati mwingi wa kuwasaidia watu kutimiza matakwa zao. Hali hii inaitwa *Nirvana*.

SWALI: Nirvana ni nini ama ni wapi?

JIBU: Hii ni mwelekeo kivukacho wakati na uwazi na hivyo ni vigumu kuzungumzia ama kuwazia, maneno na mawazo hufaa tu kufafanua mwelekeo wa nyakati - uwazi. Na kwa sababu

Nirvana iko mbele ya nyakati, hamna harakati, hamna msugvano na pia hamna kuzeeka ama mauti. Kwa hivyo *Nirvana* ni daima. Kwa sababu iko mbele ya nyakati, hamna chanzo, hamna mpaka, hamna dhana ya ubinafsi na sio ubinafsi na kwa hivyo dhana ni usio. Budha pia alituhakikishia kuwa *Nirvana* ni mapitio ya furaha tele. Alisema:

'Nirvana ni furaha ya kiwango cha juu.'

Dhp.204

SWALI: Je kunazo ushahidi kwamba mwelekeo kama huu upo?

JIBU: Hapana hamna. Lakini uwepo wake unaweza thibitishwa. Kama kuna mwelekeo ambao nyakati na uwazi hufanyika na kuna mwelekeo huo – Ulimwengu utapitia – halafu tunaweza thibitisha kwamba kuna mwelekeo ambayo nyakati na uwazi hazifanyiki – *Nirvana*. Tena, hata kama hatuwezi thibitisha uwepo wa *Nirvana*, tunazo maneno ya Buddha kuwa ipo. Alituambia:

'Kunaye Asiyezaliwa, sio Atakayekuwepo, Asiyetengenezwa, Asiye unganishwa. Kama hangekuwepo Asiyezaliwa huyu, Asiyekuwepo Asiyetengenezwa, asiye unganishwa, hakungekuwa kutoroka kwa kilichozaliwa, kilichokuwepo, kilichotengenezwa, na kilicho unganishwa. Lakini kwa sababu kunaye huyu Asiyezaliwa, asiyekuwepo, asiyetengenezwa, asiye unganishwa, kuna kutoroka kwa kilichozaliwa, kuwepo, tengenezwa na kuunganishwa.'

Ud,80

Tutalijua tukilipata. Mpaka wakati huo, bado tunaweza fanya mazoezi.

SWALI: Cheo Kikuu cha Nne cha Ukweli ni gani?

JIBU: Cheo Kikuu cha Nne cha Ukweli ni njia inayotuelekeza kuyashinda mateso. Njia hii huitwa Njia Nane Makuu na lina Kuelewa Kamili, Kuwaza Kamili, hotuba Kamili, Matendo Kamili, Maisha Kamili, Juhudi Kamili, Kukumbuka Kamili, na Makini Kamili. Maisha ya Mabuddha yahusisha kutilia maanani mambo haya nane mpaka wawe kamili. Maisha ya Ubuddha lina kufanya mazoezi hayo nane mpaka wawe kamilifu zaidi. Utagundua kwamba hatua haya zilizoko kwenye Njia Nane Makuu ya Ukweli yanatafakaria kila kipengele cha maisha: Ki akili, ki maadili, kijamii na kiuchumi, na ya kisaikolojia, na kwa hivyo ni vyenye Kila kitu mtu anahitaji kuishi maisha mema na kuendelea kiroho.

3. UBUDDHA NA WAZO LA MUNGU

SWALI: Nyinyi Mabuddha huamini kwa mungu?

JIBU: Hapana, hatuamini. Kunazo sababu nyingi kwa hii. Kama wanasosholojia na saikolojia wa kisasa, Buddha aliona kwamba wazo ya dini mingi hasa wazo la Mungu lina asili kwa wasi wasi na hofu. Buddha anasema:

‘Wakitegwa na hofu watu huenda kwenye milima takatifu, ashera takatifu, miti takatifu na mahali takatifu.’

Dhp. 188

Wanadamu wasiosahilishawa walijikuta kwenye ulimwengu hatari. Hofu ya wanyama wa pori, ya kutopata chakula tosha, ya jeraha na ugonjwa, ya matukio za kiasili kama radi, umeme na volkeno mara kwa mara ilikuwa nao. Walipokosa usalama, waliunda wazo la mungu waweze kupata faraja wakati wa dhiki, ujasiri wakati wamo hatarini na kuomboleza wakati vitu vilikwenda mrama. Mpaka leo utagundua kwamba watu huwa wenye dini sana wakati wanapokuwa kwa dhiki. Utasikia wakisema kwamba imani kwa mungu ama miungu zao huwapatia ushupavu wanayoyahitaji kupambana na maisha. Kila mara wao hueleza kwamba wanamwamini mungu fulani kwa sababu walisali wakati wa dhiki, maombi zao zikajibiwa. Haya yote yana muunga Buddha mkono kwamba wazo la mungu ni mwitikio wa hofu na kuchanganyikiwa. Buddha alitufunza kujaribu kuzielewa hofu zetu, kupunguza tamaa zetu na kwa utulivu na ujasiri tukubali vitu tusivyoweza kubadilisha. Alifufua hofu na kuelewa mantiki na imani isiyo ya akili.

Sababu ya pili Buddha hakuamini kwa mungu ni kuwa hamna thibitisho iliyotosha kuunga mkono wazo hili. Kunazo dini mingi, zote zikidai ni wao tu wanao maneno ya mungu ilyohifadhiwa kwenye vitabu vyao takatifu, kwamba ni wao tu wanaoelewa asili ya mungu, kwamba mungu yao yupo na kwamba miungu wa dini zingine hazipo. Wengine husema mungu wao ni wa kiume, wengine ni wa kike na wengine kwamba ni wastani. Wote wanaridhishwa kwamba kuna thibitisho tosha kumhusu mungu wanayemabudu lakini wanatoa umaskhara kwa thibitisho za dini

zingine kuhusu uwepo wa miungu zao. Inashangaza kwamba ingawa dini mengi wanatumia utohalisi kupitia makarne kuthibitisha uwepo wa mungu, bado hamna ukweli, saruji, kikubwa ama kisichokanushwa kwa uwepo kama huo. Mabuddha wanaahirisha hukumu mpaka thibitisho lije.

Sababu ya tatu Buddha hakuamini kwa mungu ni kwamba aliona imani kama hio haikuwa muhimu. Wengine husema kuwa imani kwa mungu ni muhimu ili kueleza asili ya ulimwengu. Lakini sayansi imeshawishi sana kueleza jinsi ulimwengu ulikuja bila kuleta wazo la mungu. Wengine husema imani kwa mungu ni muhimu ili kukuwa na maisha yenye furaha na maana. Na tena tunaweza ona ya kwamba sivyo ilivyo. Kuna mamilioni ya wakanamungu na wanaowazua uhuru, bila kutaja mabuddha wengi, wanoishi maisha muhimu, yenye furaha bila imani kwa mungu. Wengine husema imani kwenye uwezo wa mungu ndio nguvu ifaayo kwa sababu wanadamu wana udhaifu, hawana uwezo wa kujisaidia. Mara nyingine, ushahidi huo unaonyesha kinyume. Mara mingi umesikia watu walio shinda malemavu makubwa, mambo yasiyo ya kawaida na matatizo, kupitia raslimali zao za undani, juhudi zao na bila imani kwa mungu. Wengine husema mungu ni muhimu ili tupate wokovu. Lakini mjadiliano huu inafaa vizuri kama umekubali dhana za theoljia za wokovu. Na mabuddha hawakubali dhana kama hizo. Kulingana na mapitio yake Buddha aliona ya kwamba kila mwanadamu anao uwezo wa kusafisha akili zao, endeleza upendo wenye kina na huruma na kuelewa kikamilifu. Alihamasisha tahadhari kutoka mbinguni mpaka kwa moyo na kutuhimiza kupata suluhu za tatizo zetu kupitia kujifahamu – binafsi.

SWALI: Lakini kama mungu hayupo ulimwengu ulikuja aje hapa?

JIBU: Dini zote ziko na hadithi zinazojaribu kujibu swali hili. Nyakati za kale hadithi kama hizo zilitosha lakini katika karne hii ya ishirini na moja, nyakati ya fizikia, falaki, jiolojia, hadithi kama hizi zimejibiwa na ukweli wa kisayansi. Sayansi imeeleza chanzo cha ulimwengu bila kukimbilia wazo la mungu.

SWALI: Buddha anasema nini kuhusu chanzo cha ulimwengu?

JIBU: Inavutia kwamba maelezo ya Buddha kuhusu chanzo cha ulimwengu unahusiana na maelezo ya sayansi. Katika *Aganna Sutta*, Buddha alieleza dunia likiharibiwa na kufuka kwa umbo lake la sasa mamilioni ya miaka yasiyo hesabika. Maisha ya kwanza iliumbika usoni mwa maji na tena, kupitia mamilioni ya miaka, viumbe rahisi na tata zilifufika. Hizi michakato zote, alisema, bila mwanzo wala mwisho, zimewekwa kwenye mwendo na chanzo za kiasili.

SWALI: Unasema ushahidi haipo kuhusu uwepo wa mungu, na miujiza je?

JIBU: Kuna watu wengi wanao amini kwamba miujiza ni ushahidi wa kuwepo kwa mungu. Tuna sikiza madai ya kwamba uponyaji umetendeka lakini huwa hatupati ushahidi huru ya hii kutoka kwenye ofisi za matibabu ama madaktari. Tunasikiza ripoti zisizo za ukweli ya kwamba mtu aliokolewa na miujiza kutoka kwenye hatari lakini hatupati maoni za mashahidi kuhusu kile kilichotokea. Tumesikia uvumi kwamba maombi yalilainisha mwili mgonjwa ama kulainisha mguu uliokauka, lakini hatuoni eks-rei (*X-ray*) ama kupata maelezo kutoka kwenye madakatari ama wauguzi kuthibitisha uvumi haya. Ripoti porini, ripoti bandia, na tetesi sio mbadala ya ushahidi na ushahidi imara ya miujiza ni nadra. Hata hivyo, vitu visivyo vya kawaida na visivyoelezeka mara zingine hutendeka. Lakini ukosefu wetu wa kueleza mambo haya hazitoi ushahidi kwa uwepo wa mungu. Una ushahidi tu ya kwamba maarifa zetu ni duni. Kabla ya maendeleo ya dawa za kisasa, wakati watu walikosa kujua chanzo cha ugonjwa, waliamini kuwa mungu ama miungu walituma magonjwa kama adhabu. Sasa tunajua chanzo cha vitu kama hivyo na tunapokuwa wagonjwa, tunameza dawa. Wakati ambao maarifa zetu kuhusu ulimwengu sio nadra, tunaweza jua chanzo cha matukio yasiyoelezeka, jinsi tunavyojua chanzo cha ugonjwa.

SWALI: Lakini watu wengi huamini kwa mungu fulani, inaweza kuwa ukweli?

JIBU: Sivyo. Kuna wakati ambao kila mtu aliamini kwamba dunia ilikuwa sawasawa, lakini wote walikosea. Idadi ya watu wanaoamini katika wazo sio

kipimo cha ukweli ama uwongo wa wazo hilo. Njia pekee tunayoweza kusema kwamba wazo ni kweli ama sio ni kwa kuangalia na kuchunguza ushahidi.

SWALI: Sasa kama nyinyi Mabuddha hamwamini kwa mungu, mna amini kwa nini?

JIBU: Hatuamini kwa mungu kwasababu tuna amini kwa ubinadamu. Tuna amini ya kwamba kila mwanadamu ana thamani na ni muhimu, na wote wana uwezo wa kuendelea kuwa Buddha – mwanadamu kamili. Tuna amini ya kwamba wanadamu wanaweza epuka ujinga na vitu visivyo vya akili na kuona vitu jinsi vilivyo. Tuna amini kwamba chuki, hasira, licha, na wivu vinaweza chukua nafasi ya upendo, utulivu, ukarimi na uvumulivu. Tuna amini ya kwamba zote ziko kwenye fahamu ya kila mtu wakitia juhudi, wakiongozwa na kutegemea kwa Mabuddha wenzao na kutiwa na msukumo ya mfano wa Buddha. Kama Buddha anavyosema:

‘ Hakuna anayetuokoa ila sisi wenyewe,

Hakuna awezaye na atakaye weza.

Sisi wenyewe lazima tufuate njia,

Na Buddha kwa uwazi anaonyesha njia.’

Dhp.165

4. AMRI(MAAGIZO) TANO

SWALI: Dini zingine hupata mawazo zao za mema au mabaya kutoka kwa amri za mungu ama miungu zao. Nyinyi Mabuddha hamwamini mungu, sasa mnajuaje kile kizuri na kile kibaya?

JIBU: Mawazo zozote, mazungumzo ama matendo zilizopandwa kwenye ulafi, chuki na udanganyifu zinatungoza mbali na *Nirvana* na ni mabaya. Na mawazo zozote, mazungumzo ama matendo zilizo na mizizi kwa kutoa, upendo na hekima zinatungoza kusafisha njia ya *Nirvana* na ni mazuri. Kujua kilicho kizuri na kibaya kwa dini za miungu, yote yanayohitajika ni kufanya unavyoambiwa. Lakini kwenye dini la kibinadamu kama Ubuddha, kujua kilicho kizuri na kibaya, unafaa kuendeleza ufahamu binafsi wenye kina na kuelewa binafsi. Na maadili zilizotiwa kwenye kuelewa huwa zenye nguvu kuliko zenye mwitikio za amri. Sasa ili kujua kilicho kizuri ama kibaya, Mbuddha huangalia vitu vitatu - kusudi lilioko kwenye tendo, athari lenye tendo hilo litaleta kwa mtu binafsi na athari litakaloleta kwa wengine. Kama mwitikio ni mzuri (lenye mizizi ya ukarimu, upendo na hekima), Kama linanisaidia (kunisaidia kutoa mwingi, kupenda kwingi na hekima), na kusaidia wengine (kuwasaidia kutoa mwingi, kupenda kwingi na hekima), basi matendo zangu na hatua ni za kufaa, mazuri na zenye maadili. Ndio, kuna tofauti mengi ya hii. Saa zingine, natenda kwa mwitikio mwema lakini haiwezi kunifaidisha mimi binafsi ama wengine. Saa zingine mwitikio wangu ni mbali na uzuri, lakini matendo zangu husaidia wengine hata hivyo. Saa zingine natenda kwa kupitia mwitikio mwema na matendo zangu hunisaidia na pengine ni chanzo cha dhiki kwa wengine. Katika hali hizo, matendo zangu zimechanganyika – mchanganyiko wa mazuri na yasiyo mazuri sana. Kama mwitikio ni mbaya na hainisaidii binafsi wala wengine, tendo kama hilo ni mbaya. Na kama mwitikio wangu ni mzuri na inanisaidia mimi binafsi na wengine, basi tendo hilo ni nzuri kikamilifu.

SWALI: Hivyo Ubuddha una kanuni za maadili?

JUBU: Ndio inazo. Amri tano ndizo msingi za maadili za Ubuddha. Amri ya kwanza ni kuepuka kuua ama kudhuru viumbe vinavyoishi, ya pili ni kuepuka

wizi, ya tatu ni kujiepusha na utovu wa nidhamu wa kijinsia, ya nne ni kuepuka uwongo na ya tano ni kuepuka pombe na madawa za kulevya.

SWALI: Lakini kwa uhakika ni vizuri kuua saa zingine, kuua wadudu wanaoeneza magonjwa ama mtu aliyekaribia kuku ua.

JIBU: Inaweza kuwa nzuri kwako lakini kuhusu mdudu ama mtu aliye uliwa? Matakwa yao ni kuishi kama wewe. Unapoamua kuua mdudu aenezaye ugonjwa, mwitikio wako pengine ni mchanganyiko wa wasiwasi ya ubinafsi (kizuri) na kisasi (kibaya). Tendo hilo litakufaidi (Kizuri) na kwa hakika hakitamnufaisha kile kiumbe (kibaya). Sasa saa zingine ni vizuri kuua lakini sio vizuri kikamilifu.

SWALI: Nyinyi Mabuddha mna wasiwasi sana kuhusu chungu na wadudu.

JIBU: Mabuddha hujaribu kuendeleza huruma isiyobagua na inayokumbatia wote. Tunaona dunia kama ushirikiano kikamilifu penye kila kitu na kiumbe kinacho pahali pake na shughuli yake. Tuna amini kwamba kabla ya kuharibu au kusikitisha asili ya mizani, lazima tuwe waangalifu sana. Penye mkazo limetiliwa kwa kunyonya asili kwa ukamilifu, kupunguza kila tone la mwisho ndani yake bila kuweka chochote nyuma, kushinda na kutiisha, asili limekwisha kana. Hewa limetiwa sumu, mito yamechafuliwa na kufa, wanyama wengi na mimea hazipo, gange za milima yamegumba na kumomonyoka. Hata hali ya hewa inabadilika. Kama watu wangukuwa hawapondi, hawaharibu na kuua, hali hii ya kutisha haingekuwapo. Lazima tuendeleze heshima kidogo kwa maisha. Na hiki ndicho Amri ya Kwanza kinachohusu.

SWALI: Ubuddha inasema nini kuhusu utoaji mimba?

JIBU: Kulingana na Buddha, maisha yanaanza kwa kupata mimba ama baadaye kidogo, na sasa kutoa kitoto ni kuchukua maisha.

SWALI: Na kama mwanamke amenajisiwa, ama anajua mtoto wake ataumbuka, itakuwa vizuri kukomesha mimba huo?

JIBU: Mtoto aliyezaliwa kupitia ubakaji ana haki ya kuishi na kupendwa kama mtoto mwingine yeyote. Hafai kuuliwa kwa sababu baba yake mzazi alitenda uhalifu. Kuzaa mtoto aliyeumbika ama aliye na ulemavu kiakili itakuwa mgutusho cha kutisha kwa wazazi na kama kutoa mimba hivi ni sawa mbona basi hatuwai

watoto ama watu wazima walioumbika ama kupata ulemavu? Kunaweza kuwa na hali penye kutoa mimba ingekuwa suluhisho la kibinadamu, kwa mfano, kuokoa maisha ya mama. Lakini tukiwa waaminifu, mimba mengi yaliyotolewa hutendwa kwa sababu mimba hizo hazikutarajiwa, zina aibisha ama kwa sababu wazazi walitaka kuwa na mtoto baadaye. Kwa Mabuddha, hii sio suluhisho kamilifu za kuharibu maisha.

SWALI: Kama mtu amejua, atakuwa amevunja amri ya kwanza?

JIBU: Kama mtu ameua mwenzake wanaweza kulitenda kwa sababu ya hofu, hasira, ghadhabu, ulafi, ama mhemuko hasi. Kama mtu amejitoa maisha, wananfanya hivyo kwa sababu sawa ama kwasababu ya kukata tamaa ama kuchanganyikiwa. Sasa kuu ni sababu ya hisia hasi tulizoelekeza kwa wengine, na kujiua ni hisia hasi mtu anajielekeza na kwa hivyo ni kuvunja amri huo. Hata hivyo, mtu anaye tafakari kujiua ama alikuwa na jaribio la kujiua hafai kuambiwa kuwa kile alichokuwa akijaribu kutenda ni kibaya. Wanahitaji usaidizi na kuelewa kwetu. Lazima tuwasaidie kuelewa kuwa kujiua mwenyewe ni kuendeleza matatizo na sio kutatua.

SWALI: Niambie kuhusu Amri ya Pili.

JIBU: Tukichukua Amri huu tunajaribu kutochukua chochote kisicho chetu. Amri huu ni kuhusu kuzuia ulafi wetu na kuheshimu vitu vya wengine.

SWALI: Amri ya tatu inasema tunafaa kujiepusha na matendo za utadi wa ngono. Matendo za utadi wa ngono ni nini?

JIBU: Tukitumia hila, hisia za usaliti ama nguvu kumlazimisha mtu kutenda ngono na sisi, basi hiyo inaweza semwa ni matendo za utadi wa ngono. Usherati pia ni aina ya matendo za utadi wa ngono kwa sababu tunapofunga ndoa tuna ahidi mpenzi wetu kuwa tutakuwa waaminifu kwao. Tunapo husika katika usherati, tunavunja ahadi hiyo na kusaliti uaminifu wao. Ngono inafaa kuwa ishara ya upendo na urafiki kati ya watu wawili na ikiwa hivyo, inachangia kwa usawa wa kibongo na mhemuko wetu.

SWALI: Ngono kabla ya ndoa ni aina ya tendo la utadi wa kingono?

JIBU: Sio kama kuna upendo na makubaliano ya heshima kati ya wawili waliohusishwa. Hata hivyo haifai sahaulika kwamba shughuli ya kibiolojia ya ngono ni uzazi, na kama mwanamke asiye kwenye ndoa amepata mimba, inaweza sababisha kiasi kikubwa cha matatizo. Watu wengi waliokomaa na wazingativu hufikiria kwamba ni vizuri kuacha ngono mpaka baada ya ndoa.

SWALI: Ubuddha unasema nini kuhusu kudhibiti uzazi?

JIBU: Dini zingine zinafundisha kuwa kutenda ngono kwa sababu yoyote isiyo ya uzazi ni mbaya na basi hufikiria kwamba aina zote za kudhibiti uzazi kuwa si sawa. Ubuddha unatambua kwamba ngono inazo sababu kadhaa – uzazi, burudani, kama ishara ya upendo kati ya watu wawili na kadhalika. Hii ikiwa kasha, unafikiria kwamba aina zote za kudhibiti uzazi, ila utoaji wa mimba, kukubalika. Kwa kweli, Ubuddha utasema kwamba katika ulimwengu penye mlipuko wa idadi ya watu imekuwa tatizo kubwa, kudhibiti uzazi ni baraka halisi.

SWALI: Na Amri ya Nne je? Kuna uwezekano kuishi bila kusema uwongo?

JIBU: Kama kwa kweli haiwezekani kupita kwa jamii ama kufanya biashara bila uwongo, hali tatanishi kama hiyo na ya kuhusu ufidadi yafaa kubadilishwa. Mbuddha ni yule atatuaye kufanya kitu kwa vitendo kuhusu tatizo kwa kujaribu kuwa kikweli na uaminifu zaidi.

SWALI: Ukiketi kwenye bustani na mtu aliye ogopa akakupita kwa mbio, halafu tena mtu mwingine aliyebeba kisu akakukujia na kukuuliza kama umemwona alipoelekea mtu wa kwanza, utamwambia ukweli ama utamdanganya?

JIBU: Kama ningekuwa na sababu na kushuku ya kwamba mtu wa pili alikuwa akienda kumjeruhi vibaya mtu wa kwanza, ningemdanganya, kama Mbuddha mwenye akili na aliyejali, sina kusita kwa kudanganya. Tulisema hapo awali kwamba moja ya sababu zinazo amua kama kitendo ni kizuri ama kibaya ni mwitikio. Mwitikio wa kuokoa maisha ni chanya maradufu kuliko kudanganya ni hasi, katika hali kama hizi. Kama kudanganya, kulewa ama kuiba inaaminisha kwamba naweza kuokoa maisha, lazima niufanye. Mara kwa mara naweza weka marekebishio kwa kuvunja Amri haya, lakini siwezi fufua maisha kama imekufa. Hata hivyo, ilivyosemwa awali, tafadhali usichukue Amri hizi kama leseni ya

kuvunja Amri kwa wakati wowote unayofaa. Amri haya yanafaa kutumiwa kwa huduma kikubwa na zinaweza vunjwa tu kwa kesi zilizokithiri.

SWALI: Amri ya tano inasema hatufai kunywa pombe wala kutumia mihadarati. Mbona?

JIBU: Watu hawanywi kwa sababu ya ladha. Wanapokunywa pekee yao, wanatafuta kutolewa katika jitihada, na wanapokunywa kwa umaa, huwa ni kuendana. Hata kiwango kidogo cha pombe hupotosha fahamu na kuvuruga kujitambua kibinafsi. Yakiwanywa mengi, athari zake huteketeza. Mabuddha wanasema ukivunja Amri ya tano, unaweza vunja Amri zile zingine zote.

SWALI: Lakini kukunywa pombe kidogo tu haitakuwa kuvunja Amri? Ni kitu kidogo tu.

JIBU: Ndiyo, ni kitu kidogo tu na kama huwezi kutenda hata kitu kidogo, sharti na azimio yako sio lenye nguvu, ndivyo?

SWALI: Uvutaji wa sigara ni kuvunja Amri ya tano?

JIBU: Uvutaji wa sigara kwa kweli lina hasi athari kwa mwili lakini athari yake kwenye akili ni duni sana. Mtu anaweza vuta sigara na bado kuwa macho, akumbuke na kuwa sawa kibinafsi. Sasa kama uvutaji wa sigara haija ruhusiwa, itakuwa kinyume cha Amri.

SWALI: Amri Tano ni hasi. Zinatuambia zile ambazo hatufai kufanya. Hasisemi tunachofaa kufanya.

JIBU: Amri Tano ni msingi wa maadili za Ubuddha. Sizo zote. Tuna anza kwa kutambua mwenendo zetu hasi halafu kujitahidi kurekebisha. Hii ndio kazi ya Amri Tano. Baada ya kuwacha kutenda mabaya, tuna anza kutenda mazuri. Chukua kwa mfano Amri ya Nne. Budha alisema tunafaa kuanza kwa kujiepusha kusema uwongo. Baada ya hiyo, tunafaa kusema ukweli, kuongea kwa ungwana, upole na kwa wakati unaofaa.

'Kujiepusha na matamshi za uwongo, anakuwa msemaji wa ukweli; madhubuti, anayeaminika, wa kutegemewa, hadanganyi ulimwengu. Kujiepusha na matamshi za kejeli, hafanyi marudio pale kile alichokisikia hapa ili kusababisha ugomvi kati ya watu. Anawapatanisha waliogawanyika na kuwaleta pamoja wale walio

marafiki. Amani ni fahari kwake, amani ni furaha kwake, amani ni upendo kwake, ndicho kiini cha matamshi zake. Kujiepusha na matamshi za kikatili, matamshi zake haina lawama, yanaridhisha kwa sikio, yanakubalika, kwenda kwa moyo, yenye adabu na kupendwa na wengi. Kujiupusha na matamshi za uvivu, anaongea kwa wakati unaofaa, kilicho sahihi, kwa hatua, kuhusu Dhamma na kuhusu nidhamu. Anaongea maneno yanayostahili kuhifadhiwa, wakati wa lazima, yenye busara, linalo fafanuliwa vizuri na wenye hatua.'

M.I, 179

5. KUZALIWA TENA

SWALI: Sisi wanadamu tunatoka wapi na tunaenda wapi?

JIBU: Kuna majibu matatu yamkini kwa swali hili. Wale wanaoamini kwa mungu ama miungu husema kwamba kabla ya watu kuzaliwa, huwa hawako. Baadaye wanakuwepo kupitia kwa mapenzi ya mungu fulani. Wanaishi maisha zao halafu, kulingana na wanachoamini ama kufanya wakati wa maisha yao, wanaendelea aidha mbinguni milele ama kuzimu milele. Kunao wengine, watu wa utu na wanasayansi, wanaosema kuwa watu wanakuwepo wakati mimba inapatikana kwa sababu ya chanzo za kiasili, maisha, baadaye kufa, na kutoishi. Ubuddha haukubali aidha ya maelezo haya. Ya kwanza inachangia matatizo mengi za kimaadili. Kama kweli mungu mkarimu ndiye aliyemuumba kila mmoja wetu, ni vigumu kueleza kwa nini watu wengi wanazaliwa na ulemavu, ama kwa nini watoto wengi huharibika kwa mimba punde tu kabla ya kuzaliwa ama wakati wanapozaliwa. Shida nyingine na maelezo ya kiroho ni kwamba inaonekana kijeuri kwamba mtu anafaa kuteseka kuzimu kwa sababu ya walioyatenda kwa miaka 60 ama 70 ulimwenguni. Miaka 60 ama 70 ya kutoamini ama kutoishi kimaadili haifai kustahili utesaji wa milele. Vilevile, miaka 60 ama 70 ya kuishi mema inaonekana ndogo kwa furaha ya milele mbinguni. Maelezo ya pili ni bora kuliko ya kwanza na una ushahidi wa kisayansi kuliunga mkono lakini bado inawacha maswali muhimu kutojibiwa. Ni vipi tukio tata linalostaajabisha kama ufahamu wa binadamu kuendelea kuwa rahisi kama kukutana wa manii na yai, kwa muda wa miezi tisa? Na sasa utambuzi wa tawi la saikolojia, matukio kama telepathia ni ngumu kuingiza kwenye akili kilicho cha vifaa.

Ubuddha una ahidi maelezo za kurudhisha kuhusu chanzo cha wanadamu na wanapoelekea. Tunapokufa, akili na mwelekeo zake, upendeleo, uwezo, tabia zilizoendelezwa na masharti katika maisha hii, inajianzisha kwenye yai iliyorutubishwa. Hivyo mtu anakua, anazaliwa tena kuendelea kuwa na utu litekelezwayo kiakili na tabia zilizokuja kutoka kwa maisha ya kitambo na mazingira mapya. Utu huo utabadilika na kuundika kwa jitihada za ufahamu na sababu za masharti kama elimu, ushawishi wa wazazi na jamii. Wakati wa kifo utajianzisha kivyake kwenye yai lililorutubishwa. Mchakato huu wa kufa na kuzaliwa tena utaendelea mpaka chanzo cha masharti inayoisababisha, tamaa na upumbavu, zikome. Zinapokoma, badala ya kuzaliwa tena, akili hufikia hali inayoitwa *Nirvana* na hiki ndicho lengo la mwisho ya Ubuddha na maana ya maisha.

SWALI: Akili inaendaje kutoka kwa mwili moja hadi mwingine?

JIBU: Ifikirie kama wimbi za redio. Wimbi za redio, ambazo hazijatengenezwa kwa maneno ama muziki lakini kwa nguvu ya marudio tofauti, zinasambazwa, zinasonga kwenye uwazi, zinavutiwa na kuchukuliwa na kipokezi penye zinatangazwa kama maneno na muziki. Ni sawa na akili. Wakati wa kifo, nguvu za kiakili husonga kupitia kwenye uwazi na kuvutiwa na

kuchukuliwa na yai lililorutubishwa. Kiinitete kinapokua, inajivingirisha kwenye akili kwenye ina ‘tangazwa’ kama utu upya.

SWALI: Mtu huzaliwa tena kama mwanadamu?

JIBU: Hapana, kuna malimwengu mengi mtu anaweza kuzaliwa tena. Wengine huzaliwa mbinguni, wengine kuzimu, wengine wanazaliwa kama roho zenye hasira, na kadhalika. Mbinguni sio mahali pa hali ya kuwepo penye mtu anao mwili wa hila, na penye akili hupitia radhi hasa. Kama hali zote za masharti, mbinguni sio daima na kama maisha ya mtu imemalizika, mtu atazaliwa tena kama mwanadamu vizuri. Kuzimu, vilevile, sio mahali lakini hali ya kuwepo penye mtu anao mwili wa hila, na penye akili hupitia wasiwasi na dhiki. Kuzaliwa tena kama roho mwenye hasira, tena, ni hali penye mwili una hila na penye akili hupitia pigo kwa matamano na kutoridhika. Kwa hivyo, viumbe vya mbinguni hupitia radhi hasa, viumbe vya kuzimu na viumbe vyenye roho za hasira hupitia uchungu, na wanadamu huwa wanapitia mchanganyiko wa vyote. Tofauti hasa ilioko kati ya malimwengu ya kibinadamu na zile zingine ni aina ya mwili na ubora wa mapitio.

SWALI: Nini huamua pahali mtu atazaliwa tena?

JIBU: Sababu ilioko muhimu zaidi, na isiyo ya kipekee, inayoshawishi mahali tutakapozaliwa tena na aina ya maisha tutakuwa nayo, ni *kamma*. Neno *kamma* ina maanisha ‘kitendo’ na ina rejenea mwitikio wa akili na vitendo zetu. Kwa maneno mengine, kile tulicho ina amuliwa zaidi na jinsi tulivyowazua na kuyatenda zamani. Vilevile, jinsi tunavyofikiria na kutenda sasa uta athiri jinsi tutakavyokuwa wakati ujao. Mtu mungwana aliye na upendo huweza kuzaliwa tena katika malimwengu ya mbinguni, ama kama mwanadamu aliye na uhodhi wa mapitio mazuri. Mtu aliye na wasiwasi, hofu ama ukatili sana huweza kuzaliwa katika malimwengu ya kuzimu ama kama mwanadamu aliye na uhodhi wa mapitio yasiyo mazuri. Mtu anaye endelea matamano majinuni, hamu za kikatili, tamaa ya makuu zisizoweza kuridhishwa huweza zaliwa tena kama roho mwenye hasira, ama kama mwanadamu aliyechanganyikiwa na matamano na matakwa. Tabia za kiakili tunazoendelea katika maisha hii kwa urahisi zita endelea katika maisha ujao. Watu wengi hata hivyo huzaliwa kama wanadamu.

SWALI: Sasa hatuna ujasiri katika kamma yetu, tunaweza kuibadilisha.

JIBU: Ndiyo tunaweza. Hio ndio sababu moja ya hatua kwenye Njia ya Vyeo Nane ni Juhudi kamilifu. Inategemea udhati wetu, nguvu tunayoweka, ili kuyabadilisha, na kuwa waathiriwa wa matokeo zao zisizoridhisha. Watu kama hao wata endelea kuteseka mpaka watakapo badilisha tabia zao hasi. Tabia hasi hizi zinapodumu, inakuwa ni vigumu sana kuyabadilisha. Mabuddha wanaelewa hii na kuchukua manufaa ya kila nafasi kuvunja maadili za kiakili zitakazokuwa na matokeo yasiyopendeza, na kuendelea zile zitakazokuwa na matokeo zinazopendeza. Kutafakari ni moja za mbinu inayotumia mfumo wa tabia za akili, kama kwa kuingea ama kutoongea, kutenda ama kutotenda kwa njia fulani. Maisha mzima ya Mabuddha ni kujifunza kusafisha na kuweka akili kuwa huru. Kwa mfano, kama kwa kuwa mtulivu na myeyenyekevu

ulikuwa matamshi ya tabia zako katika maisha yako yaliyopita, mwelekeo kama huo itajitokeza katika maisha ya sasa. Yakihimizwa na kuendelezwa katika maisha ya sasa, zitajitokeza hata zaidi na kutamshwa katika maisha yajayo. Hii ndiyo msingi rahisi na inayo chunguliwa kikweli kwamba tabia zilizoanzishwa kitambo huwa ngumu kuvunja.

Sasa kama wewe ni mtulivu na mnyenyekevu, huwa inatendeka kwamba haufadhaishwi virahishi na wengine. Haushiki kinyongo, watu kama wewe na hasa mapitio zako huwa zenye furaha. Chukua mfano mwingine. Tuseme ulikuja kwa maisha na mwelekeo wa kuwa mtulivu na mkarimu kupitia tabia zako za kiakili za wakati uliopita. Lakini kwa maisha ya sasa uka kataa kutekeleza na kuimarisha maendeleo ya mwelekeo kama hizi. Zitakuwa dhaifu taratibu na pengine kutokuwa kabisa katika maisha yako ya wakati ujao. Utulivu na ukarimu ukidhofuka katika kesi hii, kuna uwezekano kwamba aidha maisha hii ama ujao, hamaki kiasi, na ukatili unaweza kua na kuendelea, zikija na aina zote za mapitio zisizopendeza na zinazoleta.

Tutachukue mfano moja wa mwisho. Tuseme kwamba kuhusu tabia zako za kiakili za wakati uliopita, umekuja katika maisha ya sasa na mwelekeo wa hamaki za haraka na hasira na ukagundua kuwa tabia kama hizo zina chanzo zisizopendeza. Kama unaweza kufanya mwelekeo kama hizo dhaifu, Zitakuja kwenye maisha yajayo na juhudi kiasi, yataondolewa kabisa na utakuwa uhuru kutokana na athari zao zisizopendeza.

SWALI: Umeongea sana kuhusu kuzaliwa tena, je kunazo ushahidi kwamba tunazaliwa tena tunapokufa?

JIBU: Sio tu kwamba kunazo ushahidi wa kisayansi kuunga mkono imani ya Mabuddha kuhusu kuzaliwa tena, ndiyo nadharia pekee ya baada ya maisha ambayo iko na ushuhuda yeyote kuliunga makono. Hakuna hata chembe cha ushahidi kudhibitisha uwepo wa mbinguni, ushahidi wa maangamizi wakati wa kifo unakosa. Lakini kwa miaka 30 zilizopita, tawi la kisaikolojia wamekuwa wakifanya utafiti kwamba watu wengi wako na ufahamu wa maisha zao zilizopita. Kwa mfano, huko Uingereza, msichana mwenye umri wa miaka mitano alisema aliweza kumbuka ‘mama wake mwingine na baba’, na aliongea dhahiri kuhusu kilichokuwa kama matukio kwa maisha ya mtu mwingine. Tawi la kisaikolojia waliletwa na wakauliza mamia za maswali ambazo msichana huyo alijibu. Aliongea kuhusu kuishi katika kijiji fulani kwa kile kilichokuwa kama Hispania. Alipeana jina la kijiji hicho, jina la barabara kwenye aliishi, majina ya majirani na undani kuhusu maisha yake ya kila siku huko. Pia aliongea machozi yakimtiririkia jinsi alivyogongwa na gari na kufa kwa sababu ya majeraha masiku mawili baadaye. Haya kumbukumbu yalipochunguzwa, yalipatwa kuwa sawasawa. Kulikuwa na kijiji huko Uhispania na jina ambalo huyo msichana alipeana. Kulikuwa na aina ya nyumba msichana yule alieleza na jina la barabara alichotaja. Na tena, ilipatikana kwamba mke mwenye umri wa miaka 23 aliishi kwa nyumba ile na aliuliwa miaka mitano kabla. Sasa inawezekana kwa msichana mwenye umri wa miaka 5 anayeishi Uingereza na ambaye hajawahi enda Uhispania kujua kumbukumbu kama haya? Na pia, hii siyo kesi pekee yake ya aina hii. Profesa Ian Stevenson wa Idara ya saikolojia wa Chuo kikuu cha Virginia alieleza dazeni za kesi kama hizi kwenye vitabu vyake.

Yeye ni mwanasayansi maarufu mwenye amefanya utafiti kwa miaka 25 ya watu waliokumbuka maisha zao za kitambo ni ushahidi mkubwa kuhusu funzo la Ubuddha kuhusu kuzaliwa tena.*

SWALI: Wengine wanaweza sema kwamba uwezo uliodhaniwa za maisha ya kale ni kazi za shetani?

JIBU: Hauwezi tu kukataa kila kitu kisichopata na imani yako kama kuwa kazi za shetani. Kama ukweli wa maneno magumu umetolewa kuunga mkono wazo fulani, lazima tujadili bila kufikiria na kimantiki ili kupambana nazo – sio wasiofikiria na washirikina huongea kuhusu shetani.

SWALI: Unaweza sema jadili kuhusu kuzaliwa tena ni ushirikina pia?

JIBU: Kamusi hufafanua Ushirikina kama ‘imani isiyo ya msingi ya sababu ama ukweli lakini kwa muungano wa mawazo, kama kiini macho.’ Kama unaweza kunionyesha utafiti wa taratibu ya kuwepo wa mashetani lililoandikwa na mwanasayansi, nitakubali imani huo kwa mashetani sio ushirikina. Lakini sijasikia utafiti yeyote kuhusu mashetani; wanasayansi hawawezi kufanya utafiti wa vitu kama hivyo. Sasa nasema hakuna ushahidi yeyote kuhusu kuwepo wa mashetani. Na jinsi tulivyo ona, kuna ushahidi kwamba kuzaliwa tena hufanyika. Kama uaminifu wa kuzaliwa tena ina msingi kwenye ukweli chache, haiwezi kuchukuliwa kama ushirikina.

SWALI: Vizuri, kumekuwa na mwanasayansi yeyote anayeamini kwa kuzaliwa tena?

JIBU: Ndiyo. Thomas Huxley, aliyewajibika kwa kuwasilisha sayansi kwenye mfumo wa elimu nchini uingereza katika karne ya 19, na aliyekuwa mwanasayansi wa kwanza kutetea nadharia za Darwin, aliamini ya kwamba kuzaliwa tena ilikuwa wazo nzuri. Katika kitabu chake maarufu ‘Evolution and Ethics and other Essays’, anasema:

‘Katika mafundisho ya kuzaliwa tena, chochote kilicho asili yake, Ubashiri wa Ubrahmin na Ubuddha ulipatwa, tayari kwa mkono, njia ya kujenga uthibitisho lililoaminika ya njia ya asili (Cosmos) kwa binadamu...lakini ombi hii ya uhalali haiaminiki chini kuliko zingine; na hakuna hata mmoja ila wasomi wenye pupa sana wataikataa juu ya ardhi ya asili mchanganyiko. Kama mafundisho ya mageuzi yenyewe, ile ya uhamisho (kuzaliwa tena) ina mizizi katika dunia ya ukweli; na inaweza kudai msaada kama huo kama hoja kubwa kutoka kwa kufananisha uwezo wa kusambaza.’

Profesa Gustaf Stromberg, majusi maarufu wa Sweden, mfizikia na rafiki wa Einstein pia alipata wazo la kuzaliwa upya wenye rufaa.

‘Maoni hutofautiana kama roho ya binadamu inaweza zaliwa tena duniani au la. Mwaka 1936 kesi ya kuvutia sana iliyochunguzwa na mamlaka ya serikali katika India. Msichana (Shanti devi Kutoka Delhi) aliweza kwa usahihi kuelezea maisha yake ya awali (akiwa Mutra, maili mia tano kutoka Delhi) na kumalizika mwaka mmoja kabla "kuzaliwa ya pili." Alipeana jina la mume wake na mtoto na alieleza historia ya nyumbani kwake na maisha. Tume ya kuchunguza ikamleta kwa jamaa wake wa zamani, waliothibitisha kauli yake yote. Miongoni mwa watu wa

India kuzaliwa upya huonekana kama kawaida; Jambo la kushangaza kwa ajili yao katika kesi hii ilikuwa ni idadi kubwa ya ukweli msichana alikumbuka. Hii na matukio sawa inaweza kuonekana kama ushahidi wa ziada kwa nadharia ya kutoharibika kwa kumbukumbu.’

Profesa Julian Huxley, mwanasayansi aliyejulikana Uingereza ambaye alikuwa mkurugenzi mkuu wa UNESCO aliamini kwamba kuzaliwa upya ulikuwa na maelewano na mawazo kisayansi.

‘Hakuna kitu dhidi ya kuishi kwa kudumu kwa roho binafsi kuwa katika baadhi ya njia iliyotolewa mbali baada ya kifo, kama uhakika wa ujumbe hutolewa mbali kwa kutuma vifaa vya kazi kwa namna ya pekee. Lakini ni lazima ikumbukwe kwamba ujumbe waya inakuwa ujumbe tu tena inapokuja katika kuwasiliana upya, nyenzo muundo - kipokezi. Hivyo ... kamwe haifikiri au kuhisi isipokuwa tena 'kuungana' ilivyo kwa namna fulani. Haiba zetu ziko sana kwa msingi katika mwili mpaka kweli ni vigumu kufikiria maisha itakayokuwa kweli katika maana yoyote bila mwili wa kila aina ... Naweza kufikiria kitu kupewa mbali itakayobeba uhusiano huo kwa wanaume na wanawake kama ujumbe wa waya kwa vifaa vya kupeleka; lakini katika kesi hii wafu wangukuwa, hadi sasa vile mtu anaweza kuona, ila ni misukosuko ya mifumo tofauti wakihangaika Kupitia ulimwengu mpaka ... wao ... ikarudi kweli kwa fahamu na kufanya mawasiliano na kitu kitakacho fanya kazi kama kupokea vifaa kwa ajili ya akili.’

‘Hata vitendo sana na watu wa chini duniani kama Mwanamarekani wa viwanda Henry Ford alipata wazo la kuzaliwa upya kukubalika ... Ford alivutiwa na wazo hilo kwa sababu inapatia mtu nafasi ya pili ya kujiendeleza mwenyewe. Henry Ford alisema:

‘Nilipitisha nadharia ya kuzaliwa tena nilipokuwa miaka ishirini sita ... Dini ilitoa kitu kisicho kwa uhakika ... Hata kazi haikuweza kunipatia kuridhika kamili. Kazi ni bure kama hatuwezi kutumia maarifa tunazosanya katika maisha moja hadi nyingine. Wakati niligundua kuzaliwa upya ilikuwa ni kama nilipata mpango nzima kwa ulimwengu. Nilitambua kwamba kulikuwa na uwezekano wa kutumia mawazo yangu. Muda haukuwa tena mdogo ... sikuwa tena mtumwa kwa mikono ya saa ... Fikra ni uzoefu. Baadhi wanadhani kuwa ni zawadi au kipaji, lakini ni matunda ya uzoefu wa muda mrefu katika maisha ya watu wengi. Baadhi ni nafsi wakubwa kuliko wengine, na ili waweze kujua zaidi ... Ugunduzi wa kuzaliwa upya uliweka mawazo yangu kwa urahisi ... Kama umehifadhi rekodi ya mazungumzo haya, iandike ili iweke akili ya watu katika raha. Ningependa kuwasiliana na wengine utulivu ambayo mtazamo ndefu wa maisha inatupatia.’

Hivyo mafundisho ya Mabuddha ya kuzaliwa upya una msingi wa kisayansi. Ni mantiki na kithabiti na unaendelea njia mrefu kwa kujibu baadhi ya maswali muhimu kuhusu hatima ya binadamu. Lakini pia ni faraja sana. Kwa mujibu wa Buddha, Kama ulishindwa kufikia Nirvana katika maisha haya, utakuwa na nafasi ya kujaribu tena wakati mwingine. Kama umefanya makosa katika maisha haya, utakuwa na uwezo wa kujirekebisha mwenyewe katika maisha

yajayo. Utakuwa kweli kuwa na uwezo wa kujifunza kutokana na makosa yako. Mambo hawakuweza kufanya au kufikia katika maisha haya inaweza pia kuwa inawezekana katika maisha yajayo. Mafundisho ya ajabu haya!

SWALI: Haya yote yanaridhisha kabisa kiakili lakini lazima tukubali kwamba bado nina wasiwasi?

JIBU: ‘Hiyo ni sawa. Ubuddha haidai imani kabisa katika dhana zake zote wakati zinakwenda kinyume na akili zako mwenyewe. Haja gani kuchukua hatua ya kujilazimisha mwenyewe kuamini kitu wakati katika moyo wako hutaki kuamini hivyo? Bado unaweza kufanya mambo ambayo unaona usaidizi, pitisha mawazo unazoelewa na kunufaika nazo bila kuamini katika kuzaliwa upya. Nani anajua! Kwa muda unaweza kuja kuona ukweli wa kuzaliwa upya.’

6. KUTAFAKARI

SWALI: Kutafakari ni nini?

JIBU: kutafakari ni juhudi za makusudi ya kubadili jinsi akili inavyo fanya kazi. Neno la *Pali* kwa ajili ya kutafakari ni *bhavana* ambayo ina maana ‘kufanya kukua’ ama ‘kuendeleza’.

SWALI: Kutafakari ni muhimu?

JIBU: Ndiyo. Haijalishi jinsi tunaweza kujaribu kupenda kuwa wazuri, kama hatuwezi kubadili tamaa zinazotufanya kutenda kwa njia tunafanya, mabadiliko itakuwa vigumu. Kwa mfano, mtu anaweza kutambua kwamba yeye hana utulivu kwa mkewe na aweke ahadi hivi: ‘Kuanzia sasa mimi sitakosa utulivu.’ Lakini saa moja baadaye, anaweza kuwa anamgombanisha mkewe kwa sababu tu ya kutokuwa na ufahamu wa nafsi yake, utulivu unametokea bila yeye kujua. Kutafakari husaidia kuendeleza kuelewa na nguvu inayohitajika kubadilisha tabia za akili.

SWALI: Nimesikia kutafakari inaweza kuwa hatari. Je, huo ni kweli?

JIBU: Ili kuishi, tunahitaji chumvi. Lakini kama ulikuwa unataka kukula kilo moja ya chumvi, huenda ikakuua. Ili kufanya kazi katika dunia ya kisasa unahitaji gari. Lakini kama haufuati sheria za usalama barabarani ama unaendesha ukiwa mlevi, gari linaweza kuwa mashine hatari. Kutafakari iko hivyo. Ni nzuri kwa afya zetu na ustawi wa kiakili, lakini ukifanya mazoezi kwa njia isiyostahili, inaweza kusababisha matatizo. Watu wengine wako na matatizo kama huzuni, hofu, au dhiki, na wanafikiri kutafakari ni tiba papo kwa matatizo zao. Wao huanza kutafakari na wakati mwingine matatizo zao huwa mabaya. Kama una tatizo vile, unapaswa kutafuta msaada wa kitaalamu kwanza, na kisha kuchukua kutafakari baada ya kuwa bora. Watu wengine hufikia juu matatizo zao. Wao huchukua kutafakari na badala ya kwenda hatua kwa hatua, wao hutafakari kwa nishati sana au kwa muda mrefu na hivi karibuni wao huchoka. Lakini labda matatizo zaidi katika kutafakari husababishwa na ‘aina ya kutafakari ya kangaroo.’ Baadhi ya watu huenda kwa mwalimu mmoja na kufanya kutafakari mbinu zake kwa muda.

Kisha wao husoma kitu katika kitabu na kuamua kujaribu mbinu hiyo. Wiki moja baadaye, mwalimu maarufu wa kutafakari anatembelea mji wao na hivyo wao huamua kuingiza baadhi ya mawazo zake katika vitendo vyao, na kabla ya muda mrefu wanachanganyikiwa bila matumaini. Kuruka kama kangaroo kutoka kwa mwalimu mmoja hadi mwingine, au kutoka kwa kutafakari mmoja hadi mwingine ni kosa. Lakini kama huna tatizo lolote kali za kiakili na wewe ukachukua kutafakari na mazoezi kwa waangalifu, ni moja ya mambo mazuri unayoweza kufanya kwa ajili yako mwenyewe.

SWALI: Kuna aina ngapi ya kutafakari?

JIBU: Budha alifundisha aina mingi ya kutafakari, kila imeundwa ili kuondokana na tatizo fulani au kuendeleza hali fulani kisaikolojia. Lakini mawili yaliyo ya kawaida na muhimu ni kutafakari ya ufahamu wa pumzi, *anapana sati*, na kutafakari fadhili, *Metta bhavana*.

SWALI: Kama nilikuwa nataka kufanya mazoezi ya ufahamu wa pumzi, nitaufanya namna gani?

JIBU: Unaweza kufuata hatua hizi rahisi; Ps nne - mahali (place), mkao (posture), mazoezi (practice) na matatizo (problems). Kwanza, pata mahali pa kufaa, labda chumba ambacho si pa kelele na ambapo kuna uwezekano wa kuwa bila kusikitishwa. Pili, kaa katika mkao mzuri. Njia nzuri ya kukaa ni pamoja na miguu yako mara, mto chini ya matako yako, nyuma yako sawa, mikono yako mapajani na macho yako yakifungwa. Kwa matumizi mengine, unaweza kaa kwenye kiti bora nyuma yako ikiwa sawa. Baada ya hapo kuna mazoezi halisi yenyewe. Unapokaa kimya na macho yamefungwa, ukizingatia mawazo yako ndani na nje ya harakati ya pumzi. Hii inaweza kufanyika kwa kuhesabu pumzi au kuangalia kuinuka na kuanguka kwa tumbo yako. Wakati unafanya hivyo, matatizo fulani na magumu yatatokea. Unaweza hisi kujikuna inayokera juu ya mwili wako au usumbufu katika magoti yako. Kama hali hii ikitokea, jaribu kuweka mwili wako kushirikiana bila kusonga, na kulenga pumzi. Unaweza kuwa na mawazo mengi zikija akilini mwako na bughudha kutoka kwenye pumzi. Njia pekee unayoweza kukabiliana na hii ni kwa kuvumilia kwa kurudisha mawazo yako kwa pumzi.

Ukiendelea kufanya hivyo, hatimaye mawazo itadhoofishwa, mkusanyiko yako itakuwa na nguvu na utakuwa na wakati wa kina shwari ya akili na amani ya ndani.

SWALI: Inafaa nitafakari kwa muda mgani?

JIBU: Ni vizuri kutafakari kwa dakika kumi na tano kila siku kwa wiki, na kisha kupanua muda kwa muda wa dakika tano kila wiki mpaka unatafakari kwa dakika 45. Baada ya wiki chache ya kutafakari mara kwa mara kila siku, uta anza kugundua kwamba mkusanyiko wako unakuwa bora.

SWALI: Vipi kuhusu kutafakari wa Upendo Wema? Inatekelezwaje?

JIBU: Baada ya kuzoea akili ya pumzi na unafanya mazoezi mara kwa mara, unaweza kuanza kufanya mazoezi ya kutafakari fadhili. Ni lazima kufanyika mara mbili au tatu kila wiki baada ya kufanya kukumbuka ya pumzi. Kwanza, angazia mawazo zako kwako mwenyewe na kujisemea maneno kama ‘Niwe vizuri na mwenye furaha. Niwe na amani na utulivu. Nilindwe kutokana na hatari. Mawazo yangu yawe huru kutokana na chuki. Moyo wangu ujazwe na upendo. Niwe vizuri na mwenye furaha.’ Kisha moja kwa moja fikiria mtu aliyependwa, mtu wa pande zote, mtu usiempenda ama kuchukia, na hatimaye mtu asiyependwa, ukiwatakia kila mmoja wao wema vile unajitakia.

SWALI: Aina hii ya kutafakari iko na faida gani?

JIBU: Kama unafanya Kutafakari Fadhili na tena kwa mtazamo mwema, utagundua mabadiliko chanya yanatendeka ndani yako. Utapata ya kwamba utaweza kukubali zaidi na kuwa na msamaha kuelekea kwako. Utagundua kuwa hisia unazo kuelekea kwa unaowapenda zitaongezeka. Utajipata ukiwa marafiki na watu uliotofautiana nao na kutohudumia. Na utapata nia mbaya ama chuki ulizo nazo kwa watu wengine yakipungua na hatimaye kumumunyika. Saa zingine kama unajua mtu aliye mgonjwa, asiye na furaha, ama aliye na matatizo magumu, unaweza kuwaweka ndani ya kutafakari kwako na mara kwa mara utapata hali yao ikiboreka.

SWALI: Hiyo inawezekanaje?

JIBU: Akili, ikiendelezwa vizuri, ni chombo kizuri sana. Tukijifunza kulenga nishati ya akili na kuielekeza kwa wengine, inaweza kuwa na athari juu yao. Labda umepitia kitu kama hiki. Pengine uko kwenye chumba iliyo na msongamano na ukapata hisia kwamba mtu anakuangalia. Ukageuka na, kwa ukweli, mtu anakuangalia. Chenye imefanyika ni kwamba ulichukua nishati ya akili ya yule mtu mwingine. Kutafakari Fadhili ni kama hivyo. Tunaelekeza nishati ya akili kwa wengine na unaweza kuwabadilisha hatua kwa hatua.

SWALI: Kunazo aina zozote zingine za kutafakari?

JIBU: Ndiyo. Ya mwisho na pengine ni aina ya kutafakari iliyo muhimu zaidi inaitwa *vipassana*. Neno hilo lina maanisha ‘kuona ndani’ ama ‘kuona kwa kina’.na huwa inatafsiriwa kama kutafakari ya kufahamu.

SWALI: Eleza kutafakari ya Kufahamu

JIBU: Wakati wa kutafakari ya kufahamu, mtu anajaribu tu kuwa na ufahamu ya kile kinacho watendeka bila kuifikiria au kuigusia.

SWALI: Kusudi la hiyo ni nini?

JIBU: Mara kwa mara tunaguswa na mapitio yetu kwa kuzipenda ama kutozipenda ama kuziwacha kuleta mawazo, ndoto za mchana ama kumbukumbu. Haya majibu yote yana potosha mapitio zetu kwa hivyo tunashindwa kuzielewa vizuri. Kwa kuendeleza fahamu yasiyo tendaji, tuna anza kuona kwa nini tunafikiria, ongea na kutenda tunavyotenda. Na bila shaka zaidi, maarifa za ubinafsi unaweza kuwa na athari chanya sana katika maisha zetu. Faida nyingine ya kufanya mazoezi ya ufahamu kutafakari ni kwamba baada ya muda inajenga pengo kati ya mapitio zetu na sisi wenyewe. Kisha badala ya moja kwa moja na kujibu bila uangalifu kila majaribio ama machochezi, tunaona kwamba hatuwezi kurudi nyuma kidogo, na hivyo kuturuhusu kuamua kama tunapaswa kutenda au la na kama ni hivyo ni jinsi gani. Hivyo tunaanza kuwa na udhibiti zaidi na zaidi ya maisha yetu, si kwa sababu tumeanzisha matakwa ya kichuma, lakini kwa sababu tu tunaona waziwazi zaidi.

SWALI: Sasa nitakuwa sawa nikisema ya kwamba Kutafakari ya ufahamu ni kutusaidia kuwa bora na kuwa watu wenye furaha?

JIBU: Huo ni mwanzo, mwanzo muhimu. Lakini kutafakari ina lengo ya kujivunia kuliko hiyo. Mazoezi zetu zinapokomaa na kufahamu kwetu kuwa zenye kina, tuna anza kugundua kwamba mapitio zetu si za ubinafsi, kwamba zinafanyika bila mimi kuzisababisha kutendeka na bila mimi hata kuzipitia. Hapo mwanzo anayetafakari atakuwa na mtazamo kama hizi mara kwa mara, lakini katika muda itakuwa inajitamsha zaidi.

SWALI: Huo unaonekana kutisha?

JIBU: Ndivyo , sivyo ndivyo? Na kwa kweli wakati baadhi ya watu wanapo kuwa na uzoefu huu kwa mara ya kwanza, wanaweza kuwa na hofu kidogo. Lakini hivi karibuni hofu hubadilishwa kwa utambuzi makubwa – utambuzi kwamba sio vile vimejichukua kuwa. Hatua kwa hatua uaminifu huanza kudhoofika, na kwa mda kuyeyuka kabisa, kama inavyofanyika hisia za ‘mimi’ na ‘changu’. Ni katika hatua hii ndio maisha ya Mbuddha , na kwa kweli mtazamo wao huanza kubadilika. Fikiria tu jinsi wengi binafsi, jamii, na hata migogoro ya kimataifa zina chanzo chao katika uaminifu, kwa maana ya kudhulumiwa, kufedheheshwa na kutishwa katika kilio kwaruza ‘hiki ni changu!’ ama ‘hicho ni chetu!’ Kulingana na Ubuddha, amani ya ukweli na furaha inaweza patikana tu tunapogundua utambulisho wetu. Hiki ndicho kinaitwa kuelimisha.

SWALI: Hilo ni wazo la kuvutia sana lakini pia ni ya kutisha. Jinsi gani mtu aliye elimishwa kufanya bila maana ya kujitegemea au bila hisia za umiliki?

JIBU: Vizuri, mtu aliye elimishwa anaweza kutu uliza, ‘unaweza fanyaje na maana ya kujitegemea? Unawezaje kuvumulia nonga za hofu, wivu, huzuni na kiburi, wako na watu wengine wenyewe? Hupati daima kuwa mgonjwa wa kinyang'anyiro kisichokuwa na mwisho kwa kukusanya zaidi na zaidi, ya hisia kwamba unaweza tu kupoteza zote?’ Inakaa watu walio elimishwa hufanya vizuri katika maisha. Ni wale wasioelimishwa, ‘wewe na mimi’ walio na matatizo na chanzo cha matatizo zote.

SWALI: Naona hoja lako. Lakini unafaa utafakari kwa muda mgani ndio upate kuelimishwa?

JIBU: Ni vigumu kusema na labda haina jambo. Mbona huanzi kutafakari ili uone itakupeleka wapi? Ukifanya mazoezi kwa dhati na akili, utapata inaboresha ubora wa maisha yako mno. Wakati ukipita unaweza chunguza kutafakari na *Dhamma* kwa kina. Baadaye, inaweza kuwa kitu muhimu katika maisha yako. Usianze kubashiri au kuhofika kuhusu hatua ya juu katika njia kabla hata kuanza safari. Ichukue hatua moja kwa wakati.

SWALI: Nahitaji mwalimu kunifundisha kutafakari?

JIBU: Mwalimu si muhimu kabisa lakini uongozi wa kibinafsi kutoka kwa mtu ambaye ana fahamu kwa kutafakari hakika husaidia. Kwa bahati mbaya, baadhi ya watawa na walei wanajiweka kama walimu wa kutafakari wakati wao hawajui wanachofanya. Jaribu kuchukua mwalimu ambaye ana sifa nzuri, na ambaye ana ambatana kwa karibu na mafundisho za Buddha.

SWALI: Nimesikia kwamba kutafakari inatumika sana leo na madaktari wa magonjwa ya akili na wanasaikolojia. Hii ni kweli?

JIBU:Ndiyo, ni kweli. kutafakari sasa inakubalika kama kuwa na athari zenye matibabu juu ya mawazo na hutumiwa na wafanyikazi wataalamu wengi wa akili kushawishi utulivu, kuondokana na hofu na kuleta ufahamu binafsi. Ufahamu wa Buddha wa ndani ya akili ya binadamu ni kuwasaidia watu leo kama ilivyofanya katika nyakati za kale.

7. HEKIMA NA HURUMA

SWALI: Mara kwa mara nasikia Mabuddha wakiongea kuhusu hekima na huruma. Hizi istilahi mbili zina maanisha nini?

JIBU: Baadhi ya dini huamini kwamba huruma au upendo ndizo sifa muhimu zaidi za kiroho, lakini wanashindwa kutoa kipaumbele yoyote kwa hekima. Matokeo yake ni kwamba unaweza kuishia kuwa mpumbavu mwenye roho nzuri, mtu mwema sana lakini kwa akili kidogo. Mifumo mingine ya mawazo kama sayansi, huamini kwamba hekima inaweza endelezwa wakati hisia zote, ikiwa ni pamoja na huruma, ni agizo nje ya njia. Matokeo ya hii ni kwamba sayansi imekuwa ikijifanya kwa kuchukulia zaidi matokeo. Tumesahau kwamba sayansi ni kuwatumikia binadamu, sio kudhibiti na kuwatawala. Hata hivyo, wanasayansi wameipa ujuzi wao wa kuendeleza bomu la nyuklia, na kadhalika? Ubuddha unafundisha kwamba ili kuwa mtu binafsi kweli uwiano, lazima uendeleze hekima na huruma.

SWALI: Sasa nini, kulingana na Ubuddha ni hekima?

JIBU: Hekima ya juu ni kuona kwamba katika hali halisi ya matukio zote ni pungufu, kutodumu, na si binafsi. Kuelewa huu inatuweka huru na kutuongoza kwa usalama kubwa na furaha iitwayo *Nirvana*. Hata hivyo, Buddha hakuwa na la kusema sana kuhusu kiwango hiki cha hekima. Sio hekima kama tuna amini kile tulicho ambiwa. Hekima ya kweli ni kuona na kuelewa kwa sisi wenyewe. Katika ngazi hii basi, hekima ni kuweka nia ya wazi badala ya kuwa imefungwa tukisikiliza kwa mtazamo nyingine ya maoni badala ya zetu pekee; kuchunguza kwa makini, ukweli wa mambo ambayo ni kinyume na imani yetu, badala ya kuzika vichwa vyetu kwenye mchanga; kuwa na lengo badala ya ubaguzi; kuchukua muda kuhusu maoni na imani badala ya kukubali kwanza au zaidi hisia inayotolewa kwetu. Daima kuwa tayari kubadili imani yetu wakati tumewasilishwa na ukweli inazozipinga, hii ndiyo hekima. Mtu ambaye anafanya hivi hakika ana hekima na hatimaye hufika katika ufahamu wa kweli. Njia ya kuamini kila unachoambiwa ni rahisi. Njia ya Ubuddha inahitaji, ujasiri, uvumilivu, kubadilika na akili.

SWALI: Nafikiria ni watu wachache wanaweza kufanya hivyo. Kwa hivyo mbona nichukue hatua ya Ubuddha ikiwa ni wachache tu wanaweza kufanya mazoezi hayo?

JIBU: Ni kweli kwamba si kila mtu ni tayari kwa ajili ya ukweli wa Ubuddha bado. Lakini kama mtu hakuwa na uwezo wa kuelewa mafundisho ya Buddha kwa sasa, basi wanaweza kukomaa katika maisha yajayo. Hata hivyo, kuna watu wengi ambao, kwa maneno ya haki au faraja wana uwezo wa kuongeza kuelewa kwao. Na ni kwa sababu hii Mabuddha kwa upole na kimya kimya wanajitahidi kushiriki ufahamu wa Ubuddha na wengine. Buddha alitufundisha nje ya huruma, na tunapaswa kuwafundisha wengine nje ya huruma mno.

SWALI: Nini, kwa mujibu wa Mabuddha ni huruma?

JIBU: Kama vile hekima inashughulikia upande wa akili au kufahamu ya asili yetu, huruma ni sifa ya kipekee ya binadamu. Huruma (compassion) imetengenezwa kwa maneno mawili, *co* inayomaanisha ‘ushirikiano’ na *passion* kumaanisha hisia kali.’ Na hii ndiyo maana ya huruma. Wakati tunaona mtu katika taabu na kuhisi maumivu zao kana kwamba ni zetu wenyewe, na kujaribu kuondoa au kupunguza maumivu zao, basi hiyo ni huruma. Kila la heri katika binadamu, kila sifa kama ya Buddha kama kugawa, utayari wa kutoa faraja, huruma, wasiwasi na kujali - Yote hayo ni dalili ya huruma. Utagundua kwamba katika mtu wa huruma, matunzo na upendo kwa wengine ina asili zake katika matunzo na upendo kwa ajili ya kujilinda. Tunaweza kuelewa wengine vizuri wakati sisi tunajielewa wenyewe. Tutajua nini ni bora kwa ajili ya wengine wakati tunajua nini ni bora kwa sisi wenyewe. Tunaweza kuhisi kwa wengine wakati tunapojisikia kwa wenyewe. Hivyo katika Ubuddha, maendeleo ya kiroho ya mtu kawaida humea katika wasiwasi kwa ustawi wa watu wengine. Maisha ya Buddha unaeleza kanuni hii vizuri sana. Alitumia miaka sita kujitahidi kwa ajili ya ustawi wake mwenyewe baadaye alikuwa na uwezo wa kuwa na manufaa kwa wanadamu wote.

SWALI: Sasa unasema kwamba tuna uwezo wa kusaidia watu wengine baada ya kujisaidia wenyewe. Je, huo ni uchoyo wa ubinafsi?

JIBU: Sisi kwa kawaida huona tofauti, kuwajali wengine kabla ya sisi wenyewe, kama kuwa kinyume cha ubinafsi, wasiwasi kwa ajili ya kujilinda kabla wengine. Ubuddha hauoni kama moja au nyingine lakini badala yake kama kuchanganywa

kwa yote mawili. Wasiwasi wa ubinafsi halisi hatua kwa hatua hukomaa katika wasiwasi kwa wengine, kama mtu anaona kwamba wengine ni kweli sawa na yeye mwenyewe. Hii ni huruma ya ukweli. Huruma ni kitu kizuri zaidi katika taji ya mafundisho ya Buddha.

8. ULAJI WA MBOGA

SWALI: Mabuddha wanafaa kuwa wakulaji wa mboga, sivyo?

JIBU: Sio lazima. Buddha mwenyewe hakukuwa mkulaji wa mboga. Hakufundisha wanafunzi wake wawe wakulaji wa mboga na hata leo kuna Mabuddha wengi wasiokuwa wakulaji wa mboga. Katika maandiko ya Ubudha, inasema;

'Kuwa mbaya, bila Huruma, kusengenya, kudhuru marafiki ya wengine,

kuwa bila huruma, kiburi na uchoyo-

hii inafanya mtu kuwa mchafu, si kula nyama.

Kuwa wa mambo kinyume cha maadili, kukataa kulipa madeni,

udanganyifu katika biashara, na kusababisha mgawanyiko miongoni mwa watu –

hii inafanya mtu kuwa mchafu, si kula nyama '

Sn.246 – 7

SWALI: Lakini kama unakula nyama ni wajibu wako kwa wanyama wanaouawa. Hii ni kuvunja Amri ya kwanza?

JIBU: Ni kweli kwamba unapokula nyama unawajibika kwa mauaji ya kiumbe, lakini huo ni sawa wakati unapokula mboga. Mkulima lazima anyunyizie mazao dawa ya kuua wadudu na sumu ili mboga iwasili kwenye sahani yako ya chakula cha jioni bila mashimo ndani yao. Na mara nyingine tena, wanyama wameuawa kwa kutoa ngozi kwa ukanda wako au mkoba, mafuta kwa sabuni unayotumia, na elfu ya bidhaa nyingine vilevile. Haiwezekani kuishi bila, katika baadhi ya njia, kutowajibika kwa kifo cha baadhi ya viti vingine. Hii ni mfano mwingine wa Cheo cha Kwanza cha Ukweli, kuwepo kwa kawaida ni mateso na kutoridhika. Unapochukua amri ya kwanza, unajaribu kuzuia kuwajibika kwa mauaji ya viumbe vyovyote hai.

SWALI: Mabuddha wa Mahayana hawakuli nyama.

JIBU: Hiyo siyo sahihi. Ubuddha wa Mahayana nchini Uchina waliweka mkazo mkubwa juu ya ukulaji wa mboga lakini watawa na walei wa mila ya Mahayana katika Japan, Mongolia, na Tibet kwa kawaida hula nyama.

SWALI: Lakini nadhani kwamba Mbuddha lazima awe mkulaji wa mboga.

JIBU: Kama kulikuwa na mtu ambaye alikuwa mkulaji mboga sana lakini ambaye alikuwa mbinafsi, asiyekuwa mwaminifu na ni mdhalifu, na mtu mwingine ambaye hakuwa mla mboga

lakini ambaye alikuwa anajali wengine, mwaminifu na mkarimu, nani kwa watu hawa wawili ambaye atakuwa Mbuddha bora?

SWALI: Mtu ambaye alikuwa mwaminifu na mkarimu.

JIBU: Kwa nini?

SWALI: Kwa sababu huyo mtu ni wazi na ana moyo mzuri.

JIBU: Hasa. Yule anakula nyama anaweza kuwa na moyo safi tu kama mmoja ambaye hali nyama anaweza kuwa na moyo mchafu. Katika mafundisho ya Buddha, jambo muhimu ni ubora wa moyo wako, siyo yaliyomo katika mlo wako. Watu wengi huchukua tahadhari kubwa kamwe kula nyama, lakini hawawezi kujali kuwa na wasiwasi kuhusu kuwa na ubinafsi, kutokuwa mwaminifu, ukatili au wivu. Wao hubadilisha mlo wao ambao ni rahisi kufanya wakati wanapuuzwa kubadili mioyo zao, ambayo ni jambo ngumu kufanya. Hivyo kama wewe ni mla mboga au la, kumbuka kwamba usafishaji wa akili ni jambo muhimu sana katika Ubuddha.

SWALI: Lakini kulingana na maoni ya Ubuddha, ingekuwa mtu ambaye alikuwa na moyo mzuri na alikuwa mla mboga kuwa bora kuliko mtu ambaye alikuwa na moyo mzuri lakini alikuwa mla nyama?

JIBU: Kama nia ya mla mboga mwenye roho mzuri katika kuepuka nyama ulikuwa wasiwasi kwa wanyama na sio kutaka kushiriki katika ukatili wa kilimo cha kisasa ya viwanda, kisha yeye angekuwa dhahiri anaendeleza huruma zao na wasiwasi wao kwa wengine kwa shahada ya juu kuliko mla nyama. Watu wengi hupata kwamba wanapoendelea katika *Dhamma*, wana tabia ya kawaida ya kuelekea kuwa wala mboga.

SWALI: Mtu aliniambia kuwa Buddha alifariki kutokana na kula nyama ya nguruwe lililoharibika. Ni kweli?

JIBU: Hapana sivyo. Maandiko inataja ya kwamba Buddha mwisho alikula mlo iliohusisha bakuli itwayo *Sukara maddava*. Maana ya neno hili haieleweki lakini neno Sukara ina maanisha nguruwe hivyo inaweza kumaanisha matayarisho ya nyama ya nguruwe ingawa inaweza kwa urahisi kuwa tu kama aina ya mboga, keki au kitu kingine. Kile ambacho kilikuwa, kutaja chakula hiki kimewaongoza watu wengine kufikiria kwamba kuikula kilisababisha kifo cha Buddha. Buddha alikuwa 80 wakati aliaga dunia na alikua akiugua kwa mda. Ukweli ni kwamba alikufa kwa sababu ya uzee.

9. BAHATI MZURI NA HATIMA

SWALI: Je, Buddha alifundisha nini kuhusu uchawi na uaguzi?

JIBU: Alichukua mazoea kama vile uaguzi, kuvaa hirizi za uchawi kwa ajili ya ulinzi, kupanga maeneo kwa ajili ya majengo na kupanga siku ya bahati kuwa ushirikina zisizo ya maana, aliwakataza vikali wafuasi wake kufanya mazoezi hayo. Aliita vitu hivi vyote ‘sanaa za chini.’ Anasema;

‘Ilhali baadhi ya wanaume wa kidini, wakati wanapoishi na chakula zinazotolewa na waminifu, wanaendesha maisha yao kwa zile sanaa za chini, njia hiyo ya makosa ya kuendesha maisha kama kusoma mikono, ramli kwa ishara, kutafsiri ndoto ... kuleta bahati nzuri au mbaya ... kuokota mahali penye bahati kwa ajili ya kujenga, mtawa Gotama anakataza kutoka kwa sanaa za chini, njia hiyo ya makosa ya kuendesha maisha.’

DI, 9 -12

SWALI: Basi kwa nini watu wanafanya mambo kama hayo na kuziamini?

JIBU: Kwa sababu ya ulafi, hofu uchoyo na ujinga. Mara tu watu wanapoelewa mafundisho ya Buddha, wao hutambua kwamba moyo safi unaweza kuwalinda bora zaidi kuliko vipande vya karatasi, vipande vya chuma na maneno machache zilizo imbwa. Kisha hawata tegemea mambo kama hayo tena. Katika mafundisho ya Buddha, ni uaminifu, wema, kuelewa, uvumilivu, msamaha, ukarimu na sifa zingine nzuri zinazokulinda wewe na kukupatia mafanikio ya kweli.

SWALI: Lakini baadhi ya hirizi za bahati hufanya kazi, sivyo?

JIBU: Namjua mtu ambaye huendesha maisha bora kwa kuuza hirizi za bahati. Anadai kuwa hirizi zake zinaweza kukupatia bahati nzuri, ustawi na yeye hupa dhamana kwamba utakuwa na uwezo wa kutabiri idadi ya nambari za bahati nasibu zenye zitashinda. Lakini kama anayoyasema ni kweli basi ni kwa nini mbona yeye mwenyewe sio mwenye mamilioni? Kama hirizi zake za bahati kweli zinafanya kazi, kwa nini hawezi shinda bahati nasibu ya kila wiki? Bahati pekee anayo ni kuwa kuna watu wapumbavu wanaonunua hirizi zake za uchawi.

SWALI: Kisha kunao kitu kama bahati?

JIBU: Kamusi inafafanua bahati kama ‘kuamini kwamba chochote kinachotokea, kizuri au kibaya, kwa mtu katika mfululizo wa matukio ni kutokana na nafasi, hatma au bahati.’ Buddha alikanusha imani hii kabisa. Kila kitu kinachotokea kina sababu maalum na lazima kuna baadhi ya mahusiano kati ya chanzo na athari. Kukuwa mgonjwa, kwa mfano, ina sababu maalum. Mmoja lazima awasiliane na wadudu na mwili wa mtu lazima iwe dhaifu tosha kwa wadudu kujianzisha wenyewe. Kuna uhusiano wa dhahiri kati ya sababu (wadudu na mwili dhaifu) na athari (ugonjwa) kwa sababu tunajua kwamba wadudu hushambulia viumbe na kusababisha

magonjwa. Lakini hakuna uhusiano unaoweza kupatikana kati ya kuvaa kipande cha karatasi na maneno yaliyoandikwa juu yake, na kuwa tajiri au kupita mitihani. Ubuddha unafundisha kwamba chochote kinachotokea unafanyika hivyo kwa sababu ya chanzo au sababu, na si kutokana na bahati, nafasi au hatima. Watu ambao wana nia ya bahati daima hujaribu kupata kitu - fedha kwa kawaida zaidi na utajiri. Buddha anatufundisha kwamba ni muhimu zaidi kuendeleza mioyo na akili zetu. Alisema:

'Kuwa na mafunzo ya undani na ujuzi, kuwa umefundishwa vizuri na kutumia maneno vizuri; hii ni bahati nzuri bora. Kusaidia mama yako na baba, kumshajilisha mke wako na mtoto kuwa na maisha rahisi; huu ndio bahati nzuri bora. Kuwa mkarimu, mwenye haki, kusaidia jamaa yako na kuwa mbali na hatia yoyote katika matendo ya mtu; hii ni bahati nzuri bora. Kujiepusha na uovu na kileo na kwa kuwa daima imara katika wema; hii ndio bahati nzuri bora. Heshima, unyenyekevu, ridhaa na kusikia Dhamma mema; hii ni bahati nzuri bora.'

Sn.261 -6

10. WAMONAKI NA WATAWA

SWALI: Taasisi ya kimonaki ni moja muhimu katika Ubuddha. Ni nini lengo la wamonaki na watawa na ni nini wanatakiwa kufanya?

JIBU: Madhumuni ya Buddha katika uanzilishi taratibu wa wamonaki na watawa lilikuwa ni kutoa mazingira ambayo maendeleo ya kiroho itakuwa rahisi zaidi. Jamii ya jumuiya huwatolea wamonaki na watawa mahitaji zao za msingi - chakula, mavazi, malazi na dawa - ili waweze kujitolea muda wao na utafiti kwa mazoezi ya *Dhamma*. Amri na maisha rahisi ya utawa ni mazuri kwa amani ya ndani na kutafakari. Kwa upande wao, wamonaki na watawa wanatarajiwa kushiriki wanachojua kwa jamii na kutenda kama mifano ya jinsi Mabuddha wazuri lazima waishi. Katika mazoezi halisi, lengo hii ya msingi mara nyingine imeongezwa mbali zaidi ya kile Buddha awali alitarajia na leo wamonaki na watawa wakati mwingine hutenda vitendo kama kuwa walimu wa shule, wafanyakazi wa jamii, wasanii, madaktari, na hata wanasiasa. Baadhi wamesema kuwa kuchukua majukumu hayo ni sawa kama inasaidia kukuza Ubuddha. Wengine wanasema kuwa kwa kufanya mambo kama hayo, wamonaki na watawa kwa urahisi mno hupatwa katika matatizo ya dunia na kusahau lengo la kwa nini walikwenda kwa utawa katika nafasi ya kwanza.

SWALI: Je, unastahili kuwa monaki au mtawa ndipo upate mwanga?

JIBU: Bila shaka sivyo. Baadhi ya wafuasi wa Buddha waliotimia zaidi walikuwa wanaume na wanawake wa kawaida. Baadhi yao waliendelea kiroho ya kutosha kuwafundisha wamonaki. Katika Ubuddha kiwango cha kuelewa kwa mtu ni jambo muhimu sana na ambayo haina uhusiano wowote na kama moja anavaa joho njano au suruali bluu, au kama mtu anaishi katika utawa au nyumbani. Baadhi wanaweza kupata utawa, na faida zake zote na hasara kuwa mazingira bora ya kukua kiroho. Wengine wanaweza kupata nyumba kwa furaha yake yote na huzuni, kuwa bora. Kila mtu ni tofauti.

SWALI: Kwa nini wamonaki na watawa wa Ubuddha huvaa joho ya njano?

JIBU: Wakati wahindi wa kale waliangalia katika mwitu wangeweza daima kujua majani yatakayoshuka kutoka kwenye miti kwa sababu yalikuwa aidha manjano, rangi ya machungwa, au rangi ya udongo. Kwa hiyo, nchini India njano likawa rangi ya kukataliwa. Joho ya wamonaki na watawa ni manjano ili waweze kuwa kama ukumbusho wa umuhimu wa kutoning'inia, wa kuachilia, ya kuruhusu kwenda, bila ya kusalimisha.

SWALI: Ni nini lengo la wamonaki na watawa kunyoa nywele zao?

JIBU: Kwa kawaida sisi huwa na wasiwasi sana kwa kuonekana kwetu, hasa nywele zetu. Wanawake hufikiria nywele nzuri kuwa muhimu sana na wanaume wana wasiwasi kabisa kuhusu kuwa kipara. Kuweka nywele zetu kuwa vizuri huchukua hadi mpango mzuri wa muda.

Kwa kunyoa vichwa vyao, wamonaki na watawa hujipa wenyewe muda zaidi kwa mambo ambayo ni za usaha kweli. Pia, kunyolewa kwa nywele ni mfano ya wazo la kulipa kipaumbele zaidi mabadiliko ya ndani kuliko ya nje.

SWALI: Kuwa mtawa ni vizuri sana lakini nini kitatokea kama kila mtu akawa mtawa?

JIBU: Mtu anaweza kuuliza kitu sawa kuhusu wito yoyote. ‘Kuwa daktari wa meno ni vizuri sana lakini nini kitatokea kama kila mtu akawa daktari wa meno? Hakutakuwa na walimu, wapishi, na madereva wa tekisi.’ ‘Kukuwa mwalimu ni vizuri lakini nini kitatokea kama kila mtu alikuwa mwalimu? Hakutakuwa na madaktari wa meno, na kadhalika.’ Buddha hakupendekeza kwamba kila mmoja anapaswa kuwa wamonaki ama watawa, na kwa kweli kwamba ni kamwe hakitatendeka. Hata hivyo, kutakuwa na watu ambao watawuvutiwa na maisha ya unyenyekevu na kukataliwa na wanaofurahi katika mafundisho ya Buddha juu ya zote. Na kama madaktari wa meno na walimu, wana ujuzi maalum na maarifa ambayo yanaweza kuwa na manufaa kwa jamii wanamoishi.

SWALI: Hiyo inaweza kuwa ni hivyo kwa wale wanaofundisha, kuandika vitabu au kufanya kazi za kijamii. Lakini nini kuhusu wamonaki na watawa ambao hawana la kufanya ila ni kutafakari. Ni nini mzuri wanasaidia nayo jamii?

JIBU: Unaweza kulinganisha Mtawa wa kutafakari na mtafiti wa sayansi. Jamii inasaidia mtafiti wa sayansi anapokaa maabarani mwake kufanya majaribio kwa sababu matumaini ni kwamba hatimaye atagundua au mzulia kitu ambacho kitakuwa nzuri kwa ujumla. Kadhalika, jumuiya ya Ubuddha inasaidia Mtawa wa kutafakari (na mahitaji zake ni madogo sana) kwa sababu ni matumaini kuwa atafikia hekima na ufahamu itakayokuwa nzuri kwa ujumla. Lakini hata kabla ya hii kutokea au kutotokea, mtawa wa kutafakari bado anaweza kunufaisha wengine. Katika baadhi ya jamii ya kisasa ni ‘Maisha ya Utajiri na Umaarufu’ na ubadhirifu wake, na matumizi huonekana na ubinafsi wa tamaa ambayo ulifanyika juu na ubora kufuata, au angalau kwa sababu ya wivu. Mfano kwamba kutafakari kwa Mtawa inatukumbusha kwamba mtu si lazima awe tajiri kwa kuwa na maudhui. Inatuonyesha kwamba maisha ya upole na urahisi una faida zake pia.

SWALI: Nimesikia kwamba hakuna Watawa zaidi wa Mabuddha. Hii ni kweli?

JIBU: Buddha alianzilisha utaratibu wa watawa wakati wa uhai wake na kwa miaka mia tano au mia sita, watawa walikuwa na jukumu muhimu katika kuenea na maendeleo ya Ubuddha. Lakini kwa sababu yasiyo kuwa wazi, watawa kamwe hawa kuamuru heshima sawa au kupokea msaada huo kama wamonaki; na nchini India na Asia ya Kusini, utaratibu huo ulififia. Hata hivyo, katika Taiwan, Korea na Japan, utaratibu wa watawa umeendelea kustawi. Leo katika Sri Lanka, hatua zinazochukuliwa kuanzisha tena utaratibu wa watawa kutoka Taiwan ingawa baadhi ya wanajadi wana shauku sana kuhusu hili. Hata hivyo, katika kutunza nia ya awali ya Buddha, ni haki tu kwamba wanawake na wanaume wana nafasi ya kuishi maisha ya utawa na kufaidika kutoka humo.

11. MAANDIKO ZA UBuddHA

SWALI: Karibu dini zote zina aina ya maandiko takatifu ama Bibilia. Kitabu takatifu cha Ubuddha ni gani?

JIBU: Kitabu takatifu cha Ubuddha inaitwa *Tipitaka*. Imeandikwa kwa lugha ya Uhindi ya kale inayoitwa *Pali* ambayo inakaribiana na lugha ambayo Buddha mwenyewe aliongea. *Tipitaka* ni kitabu kikubwa mno. Utafsiri wake wa Kiingereza unachukua karibu juzuu 40.

SWALI: Jina Tipitaka lina maanisha nini?

JIBU: Imeundwa kwa maneno mawili, *ti* ina maanisha ‘tatu’ na *pitaka* ina maanisha ‘kikapu.’ Sehemu ya kwanza ya jina hili inaangazia kwa ukweli kwamba maandiko za Ubuddha ina sehemu tatu. Sehemu ya kwanza, inayoitwa *Sutta Pitaka*, ina maneno za Buddha zote na vile vile vya wafuasi wake wengine walio ona mwanga. Aina ya vifaa katika *Sutta Pitaka* ni tofauti sana ambayo inairuhusu kuwasilisha ukweli ambazo Buddha alifundisha, kwa aina mbalimbali za watu. Mengi ya mafunzo za Buddha ni katika mfumo wa mahubiri na mengine katika mfumo wa majadiliano. Sehemu nyingine kama *Dhammapada* inatoa mafundisho ya Buddha kwa njia ya kati ya mashairi. *Jatakas*, kuchukua mfano mwingine, lina hadithi zinazopendeza ambapo wahusika wakuu mara nyingi ni wanyama. Sehemu ya pili ya *Tipitaka* ni *Vinaya Pitaka*. Hili lina sheria na taratibu za wamonaki na watawa, ushauri juu ya utawala wa kimonaki na utaratibu, na historia ya awali ya amri ya kimonaki. Sehemu ya mwisho inaitwa *Abhidhamma Pitaka*. Hii ni tata na jaribio ya kisasa la kuchambua na kuainisha sababu ambazo yanafanya mtu binafsi. Ingawa *Abhidhamma* ilikuja baada ya sehemu mbili za mwanzo wa *Tipitaka*, haina kitu ambacho inazipinga nazo.

Sasa kwa neno ‘*pitaka*.’ Katika India ya kale, wafanyakazi wa ujenzi walihamisha vifaa vya ujenzi kutoka sehemu moja hadi nyingine kwa njia ya kupitisha vikapu. Wangeweza kuweka vikapu juu ya vichwa vyao, kutembea umbali kidogo hadi kwa mfanyikazi mwingine, wampitishie, na atakuwa anarudia utaratibu huo. Kuandika ilijulikana nyakati ya Buddha lakini kama wastani, ilichukuliwa chini ya madhubuti zaidi kuliko kumbukumbu za binadamu. Kitabu kinaweza kuoza katika takataka ya uchafu au kuliwa na mchwa nyeupe lakini kumbukumbu ya mtu uliweza kudumu mara kwa muda mrefu kama walivyoishi. Kwa sababu hiyo wamonaki na watawa waliweka nia mafundisho ya Buddha zote kwenye kumbukumbu na kuipitisha juu kwa kila mmoja katika vikapu. Hii ndio sababu sehemu tatu za maandiko za Ubuddha zinaitwa vikapu. Baada ya kuhifadhiwa kwa namna hii kwa miaka mia kadhaa, *Tipitaka* hatimaye iliandikwa karibu 100 BC katika Sri Lanka.

SWALI: Kama maandiko yalihifadhiwa katika kumbukumbu kwa muda mrefu, ni lazima hazina uhakika sana. Mengi ya mafundisho za Buddha zingeweza kupotea au kubadilishwa.

JIBU: Utunzaji wa maandiko ulikuwa juhudi za pamoja za jumuiya ya wamonaki na watawa. Wangeweza kukutana pamoja katika vipindi vya kawaida na kuimba zote au sehemu za *Tipitaka*. Hii ulifanya kutokuwa na uwezekano kwa kitu chochote kuongezwa au kubadilishwa. Ifikirie namna hii. Kama kundi la watu mia wanajua wimbo kwa moyo na wakati wanapoiimba, mtu anapata aya vibaya au anajaribu kuingiza kifungu kipya, nini kitatokea? Idadi kamili ya wale wanaojua wimbo huo kwa usahihi watamzuia moja asiye wa kawaida kutokana na kufanya mabadiliko yoyote. Ni muhimu pia kukumbuka kwamba katika siku hizo kulikuwa hakuna televisheni, magazeti au matangazo kuvuruga akili ambayo, pamoja na ukweli kwamba wamonaki na watawa walitafakari, ilimaanisha kuwa walikuwa na kumbukumbu nzuri sana. Hata leo, kwa muda mrefu baada ya vitabu kuja katika matumizi, bado kuna watawa ambao wanaweza kutamka *Tipitaka* nzima kwa moyo. Mtawa Mengong Sayadaw wa Burma ana uwezo wa kufanya hivyo na yeye anatajwa katika Kitabu cha ‘Guinness Records’ kama kuwa bora kwa kumbukumbu duniani.

SWALI: Je, ni umuhimu gani maandiko ziko nazo kwa Mabuddha?

JIBU: Mabuddha hawafikirii *Tipitaka* kuwa usio na dosari wa ufunuo kutoka kwa mungu, kila neno ambalo wao ni lazima waamini. Badala yake, ni rekodi ya mafundisho ya mtu mkubwa ambayo inatoa maelezo, ushauri, mwongozo na faraja na ambayo inapaswa kusomwa kwa makini na kwa heshima. Lengo letu lazima ni kuelewa nini *Tipitaka* inafundisha, si tu kuamini na hivyo, kile Buddha anasema lazima iangaliwe dhidi ya uzoefu wetu. Unaweza kusema kwamba tabia sahihi ya Mbuddha kwa maandiko ni sawa kwa mtazamo wa mwanasayansi wa kufanya utafiti wa magazeti katika jarida la kisayansi. Mwanasayansi anafanya majaribio na kisha kuchapisha matokeo yake na hitimisho katika jarida. Wanasayansi wengine wataisoma kwenye gazeti na kuitibu kwa heshima lakini hawatafikiria ni halali na kuwa na mamlaka mpaka watakapokuwa wamefanya majaribio sawa na kupata matokeo sawa.

SWALI: Ulisema Dhammapada. Hiyo ni nini?

JIBU: *Dhammapada* ni moja ya kazi ndogo katika *Tipitaka*. Jina hili linaweza kutafsiriwa kama ‘Njia ya kweli’ au ‘Aya za ukweli’. Lina mistari 423, baadhi fupi, baadhi ya kushangaza, baadhi zenye rufaa za mifano, mengine wa uzuri mkubwa, kila inayozungumziwa na Buddha. Kwa sababu hiyo *Dhammapada* ni kipande maarufu ya fasihi za Ubuddha. Imetafsiriwa katika lugha kubwa zaidi na kutambuliwa kama moja ya kito ya dunia ya maandiko za kidini.

SWALI: Kuna mtu aliniambia kuwa haupaswi kamwe kuweka nakala ya maandiko juu ya sakafu au chini ya mkono wako, lakini ni lazima kuwekwa mahali pa juu. Ni kweli?

JIBU: Hadi hivi karibuni katika nchi za Ubuddha kama katika Ulaya isiyosahilishawa, vitabu vlikuwa vitu adimu na vya thamani. Kwa hivyo, maandiko daima yalikuwa yanatibiwa kwa heshima kubwa na desturi zilizotajwa ni mfano tu wa huu. Hata hivyo, wakati mila na desturi za jadi lazima bado kufuatwa, watu wengi watakubaliana kwamba njia bora ya kuheshimu maandiko za Ubuddha itakuwa kufanya mazoezi ya mafundisho zenye zimo ndani.

SWALI: Mimi napata ni vigumu kusoma maandiko za Ubuddha. Zinaonekana ndefu, kurudiwa na kuchosha.

JIBU: Tunapofungua andiko ya kidini tunatarajia kusoma maneno ya namna ya kututakasa, kutufurahisha au sifa ambayo itatuinua na kutuhamasisha. Kwa hivyo, mtu anayesoma maandiko za Ubuddha ana uwezekano wa kutoridhishwa kiasi. Wakati baadhi ya hotuba za Buddha yana ucheshi makubwa na ya uzuri, mengi yanafanana na hoja za falsafa na kufafanua maneno, kwa makini kwenye hoja, ushauri wa kina juu ya mwenendo au kutafakari, na ukweli zilizosemwa. Zinamaanishwa kukata rufaa zaidi kwa akili kuliko hisia. Tunapowacha kulinganisha maandiko za Ubuddha na zile za dini zingine tutaona kwamba wanao aina zao za uzuri - uzuri ya uwazi, ya kinaa na hekima.

SWALI: Nilisoma maandiko za Ubuddha ziliandikwa awali juu ya majani ya mitende. Kwa nini walifanya hivi?

JIBU: Wakati maandiko yaliandikwa, karatasi ulikuwa bado haijazuliwa nchini India au Sri Lanka. Nyaraka za kawaida kama barua, mikataba, akaunti na matendo ziliandikwa aidha kwenye ngozi za wanyama, karatasi nyembamba ya chuma au makuti. Mabudha hawakupenda kutumia ngozi za wanyama na kuandika maandiko juu ya mabati ingekuwa ghali na vibaya kwa hivyo matawi za mitende zilitumika. Baada ya majani kutayarishwa hasa, zilifungwa kwa kamba na kuweka kati ya mbao mbili kuzifanya rahisi na ya kudumu, kama vile kitabu ya kisasa. Wakati Ubuddha Ulikuwa Uchina, maandiko yaliandikwa juu ya hariri au karatasi. Karibu miaka 500 baadaye, haja ya kuzalisha nakala nyingi za maandiko ilisababisha uvumbuzi wa uchapishaji. Kitabu Kongwe duniani ilichapishwa katika 828 BCE, ni tafsiri ya Kichina ya moja ya hotuba za Buddha.

12. HISTORIA NA MAENDELEO

SWALI: Ubuddha sasa ni dini ya idadi kubwa ya watu katika nchi nyingi tofauti. Ilitokeaje?

JIBU: Katika kipindi cha miaka 150 ya kufariki kwa Buddha, mafundisho zake yalikuwa tayari yameenea kwa wingi Kaskazini mwa India. Kisha karibu 262 BCE mfalme wa India, Ashoka Mauriya, alijibadilisha kwa Ubuddha na kueneza *Dhamma* katika ulimwengu wake mzima. Watu wengi walivutiwa kwa kiwango cha juu cha maadili katika Ubuddha na hasa kwa upinzani wake kwa mfumo wa tabaka wa Hindu. Asoka pia aliitisha mkutano wa halmashauri kuu na kisha kuwatuma wamonaki wa kimisionari kwa nchi jirani, ambao hata walikwenda mbali kama Ulaya. Mafanikio zaidi ya ujumbe haya ilikuwa moja lililoenda Sri Lanka. Kisiwa likawa Mabudha na imebakia hivyo tangu wakati huo. Ujumbe zingine zilileta Ubuddha kusini na magharibi mwa India, Kashmir na eneo ambalo sasa ni Kusini mwa Burma na Thailand pande. Karne au zaidi baada ya hayo, Afghanistan na eneo lenye milima la kaskazini mwa India wakawa Mabudha. Wamonaki na wafanya biashara wa nchi hiyo hatua kwa hatua walichukua dini katika Asia ya kati na Uchina, kutoka ambako baadaye ilienea mpaka Korea na Japan. Ni ya kuvutia kutambua kwamba Ubuddha kweli ni mfumo tu wa kigeni wa mawazo iliyowahi kuchukua mizizi nchini China. Karibu karne ya 12, Ubuddha likawa dini kubwa ya Burma, Thailand, Laos na Cambodia, kutokana hasa na juhudi za watawa kutoka Sri Lanka.

SWALI: Ni vipi na lini Tibet likawa Mabudha?

JIBU: Katika karne ya 8 mfalme wa Tibet alimtuma balozi wa India kuleta wamonaki na maandiko za Ubudha katika nchi yake. Ubuddha ilikua juu lakini haikuwa dini kuu kutokana na sehemu na upinzani kutoka kwa makuhani wa asili ya dini ya Bon. Hatimaye, katika karne ya 11 idadi kubwa ya wamonaki wa Hindi na walimu walikuja Tibet na dini likawa imara. Tangu wakati huo Tibet imekuwa moja ya nchi nyingi zilizoweka bidii kwa Ubuddha katika dunia.

SWALI: Hivyo Ubuddha ulienea kwa upana sana.

JIBU: Si hivyo tu, kuna matukio machache sana ya Ubuddha kuwatesa dini yaliyojitokezea ilipokuwa ikienea, au kuenea kwa ushindi wa majeshi. Ubuddha daima imekuwa kuhusu njia ya upole wa maisha na wazo la kutumia nguvu au shinikizo kushawishi imani ni mbaya kwa Mabuddha.

SWALI: Ni ushawishi gani Ubuddha ulikuwa nayo kwa nchi ambazo ilienea?

JIBU: Wakati wamonaki wa kimisionari walikwenda nchi mbalimbali kwa kawaida walichukua zaidi ya mafundisho ya Buddha tu pamoja nao, walileta pia baadhi ya vipengele bora ya ustaarabu wa Hindi. Wamonaki walikuwa wakati mwingine wenye ujuzi katika dawa na walishawishi mawazo mapya ya matibabu katika maeneo ambapo yalikuwa hazijakuwepo. Wala Sri Lanka, Tibet wala mikoa kadhaa ya Asia ya kati walikuwa na maandiko mpaka wamonaki walipoianzilisha, na bila shaka kwa kuandika kulikuja maarifa mapya na mawazo. Kabla ya kuja kwa Ubuddha, Wanatibet na Wamongolia walikuwa watu wakaidi na Ubuddha uliwafanya kuwa wapole na wastaarabu. Hata ndani ya India, sadaka za wanyama ukatoka nje ya hasira kwa sababu ya Ubuddha; na mfumo wa tabaka kutokuwa mkali kiasi, angalau kwa muda. Hata leo kama Ubuddha unapoenea katika Ulaya na Marekani, saikolojia ya magharibi ya kisasa unianza kuathiriwa na baadhi ya ufahamu wake katika akili ya binadamu.

SWALI: Kwa nini Ubuddha ulififia nchini India?

JIBU: Hakuna mtu ambaye amewahi kupeana maelezo ya kuridhisha kwa ajili ya maendeleo hii ya bahati mbaya. Baadhi ya wanahistoria wanasema kuwa Ubuddha lilishapotoka kiasi kwamba watu wakageuka dhidi yake. Wengine wanasema kuwa ilipitisha mawazo mengi ya Uhindi na hatua kwa hatua kutofautishika kutoka kwa Uhindu. Nadharia nyingine ni kwamba wamonaki walianza kukusanyika katika nyumba za utawa kubwa ulio unguwa mkono na wafalme na kwamba hii iliwatengwa kutoka kwa watu wa kawaida. Sababu yoyote, karne ya 8 au 9, Ubuddha wa India ulikuwa tayari katika upungufu mkubwa. Ilitoweka kabisa wakati wa machafuko na vurugu za uvamizi wa Kiislamu wa India katika karne ya 13.

SWALI: Lakini bado kuna baadhi ya Mabudha nchini India sivyo?

JIBU: Kunazo, na kwa kweli tangu katikati ya karne ya 20 Ubuddha imeanza

kuongezeka nchini India tena. Mwaka 1956 kiongozi wa India wa tabaka lisilogusika alijibadilisha kwa Ubuddha kwa sababu yeye na watu wake waliteseka vibaya chini ya mfumo wa tabaka ya Hindu. Tangu wakati huo watu wapatao milioni 8 wamekuwa Mabuddha na idadi inaendelea kuongezeka.

SWALI: Ubuddha ulikuja magharibi lini?

JIBU: Magharibi ya kwanza ya kuwa Mabuddha pengine walikuwa Wagiriki ambao walihamia India baada ya uvamizi wa hayati Alexander katika karne ya 3 BCE. Moja ya vitabu vya kale ya Ubudha, *Milindapanha*, lina mazungumzo kati ya Mtawa wa Hindi Nagasena na mfalme wa Kigiriki Milinda. Katika nyakati za hivi karibuni mwishoni mwa karne ya 19, Ubuddha ulianza kuvutia utawala na heshima katika magharibi wakati wasomi walianza kutafsiri maandiko za Ubudha na kuanza kuandika kuhusu Ubuddha. Katika miaka mapema ya 1900 nchi za Magharibi wachache walianza kujiita wenyewe Mabuddha na moja au wawili wakawa wamonaki. Tangu miaka ya 1960 idadi ya Mabuddha kutoka magharibi wameongezeka kwa kasi na leo hii yanajumulisha wachache lakini muhimu katika nchi nyingi za magharibi.

SWALI: Unaweza sema kitu kuhusu aina tofauti za Ubuddha?

JIBU: Tangu miaka ya 1960 idadi ya Mabuddha kutoka magharibi wameongezeka kwa kasi na leo hii yanajumulisha wachache lakini muhimu katika nchi nyingi za magharibi. Aidha, ilivumulia kwa karne nyingi na ulipitisha na kukabiliana na maisha ya watu wa jamii na akili ya maendeleo. Kwa hiyo, wakati kiini cha *Dhamma* imebakia vile, hali yake ya nje ulibadilika sana. Leo kuna aina tatu kuu za Ubuddha - *Theravada*, *Mahayana*, na *Vajrayana*.

SWALI: Theravada ni nini?

JIBU: Jina *Theravada* ina maanisha mafundisho ya wazee na ni msingi zaidi juu ya *Pali Tipitaka*, iliyo kongwe na ni rekodi kamili ya mafundisho za Buddha. *Theravada* ni kihafidhina zaidi na utawa unaozingatia mfumo wa Ubuddha ambayo inasisitiza misingi ya *Dhamma* na inaelekea kuchukua mbinu rahisi zaidi na mkali. Leo *Theravada* ni mazoezi hasa katika Sri Lanka, Burma, Thailand, Laos na Cambodia.

SWALI: Ubudha wa Mahayana ni nini?

JIBU: Karibu karne ya 1 BCE baadhi ya matokeo ya mafundisho ya Buddha yalikuwa yakichunguzwa kwa undani zaidi. Pia, jamii ilikuwa ikiendelea hii ulihitaji utafsiri mpya na muhimu zaidi ya mafundisho. Shule nyingi zilizokua nje ya hayo maendeleo mapya na utafsiri kwa pamoja yaliitwa *Mahayana*, kumaanisha Njia Kuu, kwa sababu zilidai kuwa muhimu kwa kila mtu, si tu kwa wamonaki na watawa waliokuwa wamejinyima vya dunia. *Mahayana* hatimaye likawa aina kubwa ya Ubuddha nchini India na leo ni mazoezi nchini Uchina, Korea, Taiwan, Vietnam na Japan. Baadhi ya wana *Theravada* husema kwamba *Mahayana* ni upotoshaji wa mafundisho ya Buddha. Hata hivyo, Waumini wa *Mahayana* uhakika wanasema kwamba Buddha alikubali mabadiliko kama moja ya msingi zaidi ya ukweli zote na kwamba tafsiri yao ya Ubuddha hauna upotoshaji wa *Dhamma* kama mwaloni ni upotoshaji wa tunda la muoka.

SWALI: Mara nyingi nimeona neno Hinayana. Je neno huu ina maana gani?

JIBU: Wakati *Mahayana* ilikuwa inaendelea, ilitaka kujitofautisha yenyewe kutoka kwa shule ya awali ya Ubuddha hivyo ikajiita yenyewe *Mahayana*, Njia Kuu, na ikaita shule za awali *Hinayana*, kwa maana ya Njia Mdogo. Kwa hivyo, *Hinayana* ni jina fulani ya madhehebu ya kidini ambayo Waumini wa *Mahayana* huwapa waumini wa *Theravada*.

SWALI: Je kuhusu Vajrayana?

JIBU: Aina hii ya Ubuddha ulianza kuibuka nchini India katika karne ya 6 na 7 CE wakati Uhindi ulikuwa unaendeleza ufufuo kuu nchini India. Katika kukabiliana na hili, baadhi ya Mabudha walikuwa wamevutiwa na masuala ya Uhindi hasa ibada ya miungu na matumizi ya mizunguko ya mila. Katika karne ya 11, *Vajrayana* lilikuwa imara katika Tibet ambako ilifanyiwa maendeleo zaidi. Neno *Vajrayana* inamaanisha Njia ya Almasi na inahusu mantiki madhubuti kwamba *Vajrayana* ilihalalisha na kutetea baadhi ya mawazo zao. *Vajrayana* hutegemea zaidi juu ya aina ya fasihi iitwaye tantras juu ya maandiko jadi za Ubudha, na kwa hivyo wakati mwingine pia inajulikana kama *Tantrayana*. *Vijrayana* sasa ipo katika Mongolia, Tibet, Ladakh, Nepal, Bhutan na miongoni mwa Wanatibet wanaoishi nchini India.

SWALI: Hii inaweza kuchanganyisha sana. Kama nataka kufanya mazoezi za Ubudha jinsi gani naweza kujua aina ya kuchagua?

JIBU: Labda tunaweza kuilinganisha kwa mto. Kama ulienda kenye chanzo cha mto na kisha kwa mdomo wake, pengine zitatofautiana. Lakini kama ulifuata mto kutoka kwa chanzo chake, kama inapenya njia yake kupitia milima na tambarare, zaidi ya maporomoko ya maji, kupitia mito mbalimbali madogo zinazobubujika kwake, hatimaye kufika katika mdomo wake na kuelewa ni kwa nini ilionekana kuwa tofauti na chanzo. Kama unataka kujifunza Ubudha anza na mafundisho msingi za kale – Njia Nne Adimu, Njia Nane Tukufu, maisha ya kihistoria ya Buddha na kadhalika. Kisha jifunze jinsi gani na kwa nini mafundisho haya na mawazo yalifufikaje na kisha kuzingatia mbinu za Ubuddha zenye rufaa kwako zaidi. Basi itakuwa vigumu kwako kusema kwamba chanzo cha mto ni duni kwa mdomo, au kwamba kinywa ni upotoshaji wa chanzo.

13. KUKUWA MBUDDHA

SWALI: Kile umsema hadi sasa ni ya kuvutia sana kwangu. Jinsi gani naweza kuwa Mbuddha?

JIBU: Kulikuwa na mtu mmoja aitwaye Upali ambaye alivutiwa na mafundisho ya Buddha na aliamua kuwa mmoja wa wanafunzi wake. Lakini Buddha akamwambia:

‘Fanya uchunguzi sahihi ya kwanza Upali. Uchunguzi sahihi ni nzuri kwa mtu maalum kama wewe mwenyewe.’

M.II,379

Katika Ubuddha, kuelewa ni muhimu sana na kuelewa inachukua muda. Ni bidhaa mwisho wa mchakato, hivyo usikimbilie katika Ubuddha kwa hamu. Chukua muda wako, uliza maswali, fikiria kwa makini na kisha fanya uamuzi wako. Buddha hakuwa na nia ya kuwa na idadi kubwa ya wanafunzi. Alikuwa na wasiwasi kwamba watu wanapaswa kufuata mafundisho yake kutokana na uchunguzi wa kimakini na kuzingatia ukweli.

SWALI: Kama nimefanya hivi na kupata mafundisho ya Buddha kukubalika, nitafanya nini basi kama nilitaka kuwa Mbudha?

JIBU: Itakuwa bora kujiunga na hekalu nzuri au kundi la Ubuddha, wape msaada wako, unywa mikono nao na endelea kujifunza zaidi kuhusu mafundisho ya Buddha. Kisha, wakati umekuwa tayari, utakuwa Mbuddha rasmi kwa kuchukua Makimbilio Matatu.

SWALI: Makimbilio matatu ni nini?

JIBU: Kimbilio ni mahali ambapo watu huenda wanapokuwa na shida au wakati wanahitaji usalama au kulindwa. Kuna aina nyingi za kimbilio. Wakati watu wako mashakani wao hukimbilia kwa marafiki zao. Buddha alisema:

‘Kupata kimbilio katika Buddha,

Dhamma na Sangha na

kuona kwa akili halisi

Vyeo Nne Kweli za Adimu,

mateso, chanzo cha mateso,

kuvuka mateso na

Njia ya vyeo Nane inayoongoza

kuvuka mateso

Hii kweli ni marejeo salama,

hii ni kimbilio ya juu kabisa.

Hii ni kimbilio ambapo moja ana

kuwa huru kutokana na mateso yote.'

Dhp. 189- 192

Kuchukua kukimbilia katika Buddha ni kukubali kwa uhakika wa ukweli kwamba mtu anaweza kuwa kikamilifu kwa mwanga na kukamilishwa tu kama Buddha alikuwa. Kuchukua kukimbilia katika *Dhamma* ina maana ya kuelewa Ukweli Nne Adimu na kuweka msingi wa maisha ya mtu katika Njia Tukufu Nane. Kuchukua kukimbilia katika *Sangha* ina maanisha kutafuta msaada, kutia msukumo na uongozi kutoka kwa wote wanao tembea kwa Njia Tukufu Nane. Kwa kufanya hivyo, moja anakuwa Mbuddha na hivyo anachukua hatua ya kwanza katika njia ya kuelekea *Nirvana*.

SWALI: Ni mabadiliko magani yametokea katika maisha yako tangu kuchukua kwanza Kimbilio Matatu?

JIBU: Kama mamilioni wengine zaidi ya miaka 2500 iliyopita, mimi nimegundua kwamba mafundisho ya Buddha yamefanya hisia nje ya dunia mgumu. Yametoa maana kwa maisha yasiyokuwa ya maana. Yameniletea utu na maadili za huruma ambayo inaniongoza kuishi maisha yangu, na yamenionyesha jinsi naweza kufikia hali ya usafi na ukamilifu katika maisha yajayo. Mshairi nchini India ya kale mara moja aliandika kumhusu Buddha:

'Kwa kwenda kwake kwa kumkimbilia, kuimba sifa zake, kumfanyia heshima na kukaa katika Dhamma yake ni kutenda kwa akili.'

Nakubaliana na maneno haya kabisa.

SWALI: Nina rafiki ambaye daima hujaribu kunibadili. Kwa kweli sina nia ya dini yake na nimemwambia hivyo lakini hataki kuniwacha peke yangu. Naweza kufanya nini?

JIBU: Jambo la kwanza kuelewa ni kwamba mtu huyu si kweli rafiki yako. Rafiki wa kweli anakupokea jinsi ulivyo na kuheshimu matakwa yako. Mimi namshuku mtu huyu kujifanya kuwa rafiki yako ili aweze kukubadilisha wewe. Wakati watu wanajaribu kulazimisha mapenzi yao juu yako, wao kwa hakika sio marafiki zako.

SWALI: Lakini anasema anataka kushiriki dini yake na mimi.

JIBU: Kushiriki dini yako na wengine ni jambo nzuri lakini naona kwamba rafiki yako hajui tofauti kati ya kugawa na kuweka. Kama nina tunda la tufaha, nikakutolea nusu na ukakubali, basi nimegawana pamoja na wewe. Lakini ukiniambia ‘Asante, lakini tayari nimekula’ na nikaweka kuisitiza kwamba uchukue nusu ya tufaha mpaka hatimaye ukakubali kutokana na shinikizo langu, hii ni vigumu kuitwa kugawana. Watu kama 'rafiki' yako hujaribu kuficha tabia zao mbaya na kuiita ‘kugawana’ ‘upendo’ au ‘kushuhudia.’ Kwa jina lolote wanaloliita, mienendo yao bado ni ya kifidhuli, mbaya kiadabu na ubinafsi.

SWALI: Hivyo ni jinsi gani naweza kumzuia?

JIBU: Ni rahisi. Kwanza, kuwa wazi katika akili yako unchotaka. Pili, kwa wazi na ufupi mwambie hivyo. Tatu, wakati anauliza maswali kama ‘ imani yako ni nini juu ya jambo hili’ au ‘kwa nini hutaki kuja kwenye mkutano na mimi,’ kwa wazi na upole na endelea kurudia kauli yako ya kwanza. ‘Asante kwa mwaliko lakini afadhali nisikuje.’

‘Kwa nini?’

‘Hiyo kwa kweli ni biashara yangu. Afadhali nisikuje.’

‘Kutakuwa na watu wengi wa kuvutia huko.’

‘Nina hakika kutakuwa na lakini afadhali nisikuje.’

‘Mimi nakukaribisha kwa sababu nakujali.’

‘Nafurahi unanijali lakini afadhali nisikuje.’

Kama kwa wazi, uvumilivu na kuendelea kujirudia mwenyewe na kukataa kumruhusu kushiriki katika majadiliano, hatimaye atakata tamaa. Ni aibu kwamba unafaa kufanya hivyo, lakini ni muhimu sana kwa watu kujifunza kwamba hawawezi kulazimisha imani zao au matakwa juu ya wengine.

SWALI: Mabudha wanafaa kujaribu kushiriki Dhamma na wengine?

JIBU: Ndiyo ni lazima. Kama watu wanakuuliza kuhusu Ubuddha, waambie. Unaweza hata kuwaambia kuhusu mafundisho ya Buddha bila ya wao kuuliza. Lakini kama, kwa aidha maneno yao au vitendo vyao, wakikujulisha hawana nia, kukubali hiyo na heshimu matakwa yao. Ni muhimu pia kukumbuka kwamba wewe unafaa kuruhusu watu kujua kuhusu *Dhamma* mbali kwa ufanisi zaidi kwa njia ya matendo yako na si kupitia mahubiri yako kwao. Onyesha watu *Dhamma* daima kwa kuwa mpole, mwema, mvumilivu, mwenye haki na mwaminifu. Wacha *Dhamma* *kuangaza* kupitia maneno na matendo yako. Kama kila mmoja wetu, wewe na mimi, wananajua *Dhamma* kabisa, mazoezi yake kikamilifu na kushiriki kwa ukarimu na wengine, tunaweza kuwa na faida kubwa kwa wenyewe na kwa wengine pia.

14. MISEMO ZINGINE ZA BUDDHA

Hekima ni kujitakasa kwa fadhila na fadhila kwa hekima. Penye kuna moja mara zote kuna mwingine. Mtu mwema ana hekima na mtu mwenye busara ana fadhila. Mchanganyiko wa mawili unaitwa kitu cha juu zaidi duniani.

D.I,84

Akili huendeleza mambo zote, akili huzitawala, zote zimeundwa kiakili. Kama mtu anaongea au kutenda kwa nia safi, furaha huwafuata kama kivuli kisichowaacha.

Dhp.2

Mtu hapaswi kumlaumu mwingine au kumdharau mtu yeyote mahali popote kwa sababu yoyote. Usimtakie maumivu mwingine nje ya aidha hasira au upinzani.

Sn.149

Kama vile bahari kuu ina ladha lakini moja, ladha ya chumvi, hivyo pia hii Dhamma ina ladha lakini moja, ladha ya uhuru.

Ud.56

Ni rahisi kuona makosa za wengine lakini ni vigumu kuona zako mwenyewe. Wakati tunapepeta makosa za wengine kama makapi, sisi huzijificha zetu wenyewe kama mwindaji anayejificha mwenyewe katika mafichoni. Wale ambao huangalia makosa za wengine hupata tu hasira. Hasi zao hua ni mbali kwa kuharibiwa.

Dhp.252-3

Taji za maua mengi zinaweza kufanywa na chungu ya maua. Kadhalika, matendo mengi mazuri yanaweza kutendwa na mtu moja binadamu aliyezaliwa.

Dhp.53

Wakati unzungumza na watu wengine unaweza kusema kwa wakati unaotakiwa au wakati usiofaa, kwa mujibu wa ukweli au la, kwa upole au vibaya sana, kwa uhakika au la, kwa akili kamili ya chuki au upendo. Unapaswa kujifundisha mwenyewe kama hivi; ‘Akili zetu haitapotoshwa wala kusema hotuba mabaya bali kwa wema na huruma, tutaishi kwa akili huru kutoka chuki na kujazwa na upendo. Tutaishi tukimfaidisha kwanza mtu mmoja kwa upendo na kwa kuanzia na wao, tufaidishe dunia nzima kwa upendo uliojitana, uliokithiri, isiyo na kipimo na kabisa bila ya chuki au uadui.’ Hivi ndivyo unavyopaswa kujifundisha mwenyewe.

M.I,126

Ni kwa mambo matatu ambayo mtu mwenye busara anaweza kutambuliwa. Matatu magani? Anaona makosa yake mwenyewe jinsi ilivyo, juu ya kuziona anajaribu kuzisahihisha, wakati wengine wanatambua makosa zao yeye huwasameheha.

A.I,103

Acheni kutenda mabaya, jifunze kutenda mema, safisha akili. Hii ni mafundisho ya Mabuddha.

Dhp.183

Jifunze hii kutoka kwenye maji. katika mlima nyufa na mapengo, mafuriko makubwa mkondo yatoa. Lakini mito kubwa hububujika kwa kimya. Mambo matupu hufanya kelele, kilicho jaa siku zote hutulia. Mjinga ni kama mtungi uliojazwa nusu, mtu mwenye busara kama kisima cha kuogolea kisicho na kina.

Sn.720-1

Hata kama wahalifu wa chini walikuwa wakukate mguu kwa mguu na msumeno yenye meno maradufu, kama unjaza akili yako na chuki hutakuwa unafanya mazoezi ya mafundisho yangu.

M.I,126

Kama mmoja ana wivu, uchoyo au kutoaminika wao hawapendezi licha ya ufasaha wao na sifa nzuri. Lakini mtu ambaye ni safi kutoka kwa mambo kama hayo ni huru kutoka kwa chuki, ni yeye anayependeza.

Dhp.262-3

Haiwezekani kwamba mtu ambaye si mwenyewe kuzuiwa, kuwa na nidhamu au kuridhika kuweza kujizua, nidhamu au kukidhi wengine. Lakini inawezekana kabisa kwamba mtu ambaye amejizua, kuwa na nidhamu na kujikidhi wenyewe, wanaweza kusaidia wengine kuwa kama hivyo.

M.I,45

Kuridhika ni utajiri mkubwa.

Dhp.204

Ikiwa wengine wananikosoa, Dhamma au Sangha, hupaswi kupata hasira au kulipa kisasi kwa sababu ambayo ingeweza weka wingu kwenye hukumu lako na hutajua kama kile alisema ilikuwa sahihi au makosa. Ikiwa wengine wanafanya hivyo, waeleze jinsi upinzani wao sio sahihi, ukisema, 'Hii sio sahihi. Hiyo siyo haki. Hii sio njia yetu. Hivyo sivyo tunavyofanya.' Kadhalika, kama wengine wananisifu au Dhamma au Sangha, hupaswi kupata kiburi au majivuno kwa sababu ambayo ingeweza weka wingu kwa hukumu yako na hutajua kama kile

alisema ilikuwa sahihi au makosa. Hivyo kama wengine wanafany hivi waelezee jinsi sifa zao ni za haki, na kusema, 'Hii ni sahihi. Huo ni sahihi. Hii ni njia yetu. Hiyo hupatikana kwetu.'

D.I,3

Kama maneno yana alama tano hayasemwi kwa ubaya, inayofaa kupongezwa na kusifiwa na wenye busara. Matano magani? Yanasemwa wakati unaofaa, ni za ukweli, zinasemwa kwa upole, na kwa uhakika, na zinasema kwa upendo.

A.III, 243

Kama vile ziwa wenye kina ni wazi na kutulia, hata hivyo wenye busara huwa kabisa kwa amani wanaposikia mafundisho.

Dhp.82

Ni wa umuhimu kidogo kupata hasara ya mambo kama vile utajiri, lakini ni jambo la kutisha kupoteza hekima. Ni wa muhimu kidogo kupata mambo kama vile utajiri, lakini ni jambo la ajabu kwa kupata hekima.

A.I,15

Kusoma maandishi matakatiifu na kutozingatia kinachosema ni kuwa kama mchungaji wa ng'ombe anaye hesabu ng'ombe za mwingine na kukosa faida ya maisha matakatiifu.

Dhp.19

Kama vile mama humlinda mtoto wake wa pekee hata katika hatari ya maisha yake, hivyo pia, mtu anatakiwa kuwa na upendo usio na kikomo kwa viumbe vyote duniani.

Sn.150

Mtu ambaye anataka kushauriana na mwingine lazima kwanza atafakari namna hii; 'mimi ndiye ama mimi siye yule atendaye usafi kamili katika mwili na katika hotuba?' 'Sifa hizi ziko kwangu au la?' Kama hazipo, kutakuwa hamna shaka kuwa wale wanaosema; 'kuja sasa, kwa nini hamfanyi mazoezi safi kamili katika mwili na hotuba ya kwanza?' Tena, mtu ambaye anataka kushauriana na mwingine lazima kwanza atafakari kwa namna hii; 'Je, niko huru mwenyewe kutoka kwa nia mbaya na kuendeleza upendo kwa watu wengine? Sifa hizi ziko ndani yangu au la?' 'Kama hazipo, kutakuwa hakuna shaka kuwa wale wanaosema; 'kuja sasa, kwa nini hufanyi mazoezi za upendo mwenyewe?'

A.V,79

Kila atendaye haki asubuhi, saa sita mchana au usiku, watakuwa na furaha asubuhi, furaha saa sita mchana na furaha usiku.

A.I, 294

Kama mtu anakutusi, anakupiga wewe, kukutupia mawe au kukuchapa kwa fimbo au upanga, lazima kuweka tamaa za dunia na masuala kando na kufikiri, 'Moyo wangu haitasukumwa. Mimi sitasema maneno mabaya. Sitahisi chuki lakini kudumisha wema na huruma kwa viumbe wote. Unapaswa kufikiria kama hivi.'

M.I,126

Wamwagiliaji huongoza maji, kufyonza mkunjo shimoni, seremala hulainisha mbao, wenye busara hujilainisha wenyewe.

Dhp.80

Kuna aina nne ya watu wanaopatikana duniani. Wanne wagani? Wale wasio na wasiwasi kwa ustawi wao wenyewe au ustawi wa watu wengine, wale walio na wasiwasi kwa ustawi wa watu wengine lakini sio kwao wenyewe, Wale wanaohusika na ustawi wao wenyewe lakini si kwa wengine, na wale ambao wana wasiwasi kwa ustawi wao wenyewe na ustawi wa watu wengine... Kati ya aina ya watu wanne hawa, wale ambao wana wasiwasi na ustawi wao wenyewe na ustawi wa watu wengine ni wakuu, wako juu, juu kabisa na walio bora.

A.II,94

Kama wewe unachukua kukimbilia katika Buddha, Dhamma na Sangha utakuwa huru kutoka kwa hofu na kutetemeka.

S.I,220

Shinda chuki kwa upendo, ubaya kwa wema, udhaifu kwa ukarimu na uongo kwa ukweli.

Dhp.223

Wale ambao mawazo zao, maneno na matendo ni mazuri ni rafiki bora kwa wenyewe. Hata kama wanasema, 'Hatujali kuhusu sisi wenyewe' bado ni rafiki bora kwao wenyewe. Na ni kwa nini? Kwa sababu wao hujfanyia wenyewe kile ambacho rafiki anaweza kufanya kwa ajili yao.

S.I71

Usidhani kwa wepesi kuhusu wema ukisema, 'siwezi kuwa hivyo.' Tone kwa wakati mtungi wa maji hujaa na kadhalika kidogo kidogo wenye busara hujijaza wenyewe kwa wema.

Dhp.122

Sasa wakati huo Mtawa mmoja alikuwa anasumbuliwa na ugonjwa wa kuhara damu na alilala mahali ambako alikuwa ameanguka katika kinyesi chake mwenyewe. Bwana na Ananda

walikuwa wanatembelea makazi na wakaja ambapo Mtawa mgonjwa alikuwa na Bwana akamuuliza; ‘Mtawa, nini ni mbaya na wewe?’

‘Naendesha Bwana.’

‘Je, hakuna mtu yeyote anayeweza kukuangalia wewe?’

‘Hapana Bwana’

‘Na mbona watawa wengine hawawezi kukuangalia?’

‘Kwa sababu mimi ni sina matumizi kwao.’

Bwana akamwambia Ananda; ‘Nenda uchote maji na tutamwosha Mtawa huyu.’ Hivyo Ananda akaleta maji na Bwana alimwaga maji wakati Ananda anamwosha Mtawa kote. Kisha wakambeba Mtawa kwa kichwa na miguu wakamchukua na kumlaza juu ya kitanda. Baadaye Bwana aliwaita watawa pamoja na kuwauliza; ‘Kwa nini hamkuangalia mtawa mgonjwa?’

‘Kwa sababu alikuwa hana matumizi kwetu.’

‘Watawa, hamna mama au baba kuwatunza nyinyi. Kama hamuangalii baada ya kila mmoja, ni nani mwingine ataweza? Yule ambaye anaweza kuwa muuguzi wangu basi huyo ni muuguzi wa wagonjwa.’

Vin.IV,301

Zawadi ya kweli ni bora unaozidi zawadi nyingine zote

Dhp.354

Ni vizuri mara kwa mara kufikiria kuhusu makosa yako mwenyewe.

Ni vizuri mara kwa mara kufikiria kuhusu makosa ya wengine.

Ni vizuri mara kwa mara kufikiria kuhusu fadhila zako. Ni

vizuri mara kwa mara kufikiria kuhusu fadhila za wengine.

A.V,159

Wale wanaofanya vizuri hufurahi sasa, hufurahi baadaye, hufurahi sasa na baadaye. Wanafurahia na wana furaha wakati wanafikiria matendo yao mema.

Dhp.16

Epukeni mabaya. Inaweza kufanyika. Kama ingekuwa vigumu singekuuliza wewe kufanya hivyo. Lakini inawezekana na kwa hivyo ninasema, 'Epukeni mabaya.' Kama kuepuka mabaya imesababisha hasara kwako na huzuni singeweza kukuuliza wewe kufanya hivyo. Lakini itakuwa kwa ajili ya ustawi wako na furaha na hivyo nasema 'Epukeni mabaya.' Boresha uzuri. Inawezekana. Kama ingekuwa ni vigumu singekuuliza wewe kufanya hivyo. Lakini inawezekana na kwa hiyo nasema, 'Boresha uzuri.' Kama kuboresha uzuri imesababisha hasara na huzuni kwako singependa kukuuliza wewe kufanya hivyo. Lakini itakuwa inaboresha ustawi wako na furaha na hivyo nasema, 'Boresha uzuri.'

A.I,58

Wote hutetemeka katika adhabu, maisha ni mapenzi kwa wote. Kwa hiyo, jiweke mwenyewe katika nafasi ya wengine na usiuwe wala kufanya mzaha ya mauaji.

Dhp.130

Kama Himalaya, mazuri huangaza kutoka mbali. Kama mshale ulioachiliwa katika usiku, mbaya ni wasio na cheo.

Dp.304

Bwana akasema; 'Unafikira nini kuhusu hili? Lengo la kioo ni nini?' 'Ni kwa lengo la kuonesha,' akajibu Rahula. Kisha Bwana akasema; 'Hata hivyo, hatua kifanyike kwa mwili, hotuba au mawazo tu baada ya kutafakari kwa makini.'

M.I.415

Kama vile Mto Ganges inatiririka kuelekea, inajielekeza kuelekea, inaelekea upande wa mashariki, hivyo pia, yule anayelima na kuendeleza Njia Nane Tukufu anatiririka kuelekea, anajielekeza kuelekea, kuelekea Nirvana.

S.V,40

Wale ambao wanashika kufikiri, 'Alinitusi!' 'Alinipiga!' 'Alinidhulumu!' 'Ameniiba!' kamwe bado kutuliza chuki zao. Na wale wanao wacha mawazo haya wataweza. Kwa katika dunia hii chuki kamwe haitulizwi na chuki zaidi. Ni upendo ambao unatuliza chuki. Huu ni ukweli wa milele.

Dhp.3-5



Mheshimiwa Shravasti Dhammika alizaliwa nchini Australia na akawa mumonaki nchini India mwaka 1976. Amekuwa akiishi nchini Sri Lanka na Singapore kwa miaka mingi na ni mwandishi wa vitabu mbalimbali juu ya Ubuddha na masomo yanyohusisha Ubuddha. Katika kitabu hiki Mheshimiwa Dhammika anapeana majibu wazi, kwa uzingativu na ya kuchangamsha kwa majibu ya maswali zaidi ya 130 yanayo ulizwa kwa kawaida kuhusu Ubuddha.